**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 7.Mhe. Soud Yussuf Mgeni | Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Wawi. |
| 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 9.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 15.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 16.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 20.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 21.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 25.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 27.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 28.Mhe. Omar Ali Shehe | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 29.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Abass Juma Muhunzi | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Chambani. |
| 31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 32.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Jimbo la Mkanyageni. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 35.Mhe. Said Ali Mbarouk | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Gando. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 44.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 45.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |
| 46.Mhe. Ali Moh’d Bakari | Jimbo la Tumbe. |

| | |
|---|---|
| 47.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 48.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 49.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 52.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 53.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 54.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 55.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 57.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 58.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 59.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 60.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 61.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 62.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 63.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |
| 64.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 65.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |

| | |
|---|---|
| 67.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 68.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 69.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 70.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 71.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 72.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 73.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 74.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |
| 75.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Nafasi za Wanawake. |
| 76.Mhe. Zahra Ali Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| **Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Sita – Tarehe 28 Januari, 2009**

*(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti, (Ali Mzee Ali) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 88**

**Ufumbuzi wa Kero za Muungano**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin -** Aliuliza**:-**

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipokuwa akilihutubia Bunge katika Mkutano wa bajeti wa 2008 – 2009, huko Dodoma, aliwaelezea Wabunge mafanikio yaliyopatikana katika maendeleo ya vikao vya kero za Muungano kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, na kueleza kuwa mambo kumi yameweza kupatiwa ufumbuzi na mengine bado yanaendelea kushughulikiwa.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni mambo yepi kumi yaliyopatiwa ufumbuzi hadi sasa ?

(b) Kwa kuwa kero kumi zishapatiwa ufumbuzi, Je ni kero ngapi zinaendelea kushughulikiwa ?

(c) Je, serikali inaahidi lini kero hizo zilizobakia zitakuwa zimeshapatiwa ufumbuzi ?

**Mhe. Waziri Kiongozi -** Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake Nam. 88 kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kutatua kero zilizomo ndani ya Muungano, Viongozi Wakuu wa Kitaifa wamechukua juhudi tofauti ikiwa ni pamoja na kukaa vikao vya kujadili kero hizo. Miongoni mwa vikao hivyo ni vikao vya Waziri Mkuu chini ya Uwenyekiti wa Mhe. Makamo wa Rais.

Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Mhe. Rais amezungumza, lakini haikuwa na maana kuwa mambo 10 yameshapatiwa ufumbuzi bali mambo yote yanayozungumzwa katika vikao hivyo ya kero za Muungano ni kumi. Kwa hivyo si kama alivyouliza Mheshimiwa kuwa masuala 10 yameshapatiwa ufumbuzi na masuala mengine yanaendelea kushughulikiwa.

Isipokuwa mpaka sasa hivi mambo yaliyopatiwa ufumbuzi ni masuala mawili tu ambayo kwa baadaye nitayaeleza. Labda niyataje mambo hayo kumi ambayo yanayojadiliwa katika vikao vyetu vya kero za Muungano ni :-

1. Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binaadamu. Suala hili tayari limeshapatiwa ufumbuzi na jambo ambalo limebakia ni kutengeneza Kanuni na hizo kanuni kwa taarifa za hizi karibuni zimeshakamilika. Kwa hiyo tunategemea katika vikao vyetu vya vitakavyokuja vya kero za Muungano mwezi wa Febuari suala hili litakuwa linaondoka katika agenda.

2. Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mshariki. Suala hili bado tunaendelea kulizungumza na bado mazungumzo ni mazito lakini yanaendelea vizuri.

3. Utafutaji na Uchimbaji wa mafuta na Gesi Asilia. Suala hili kama tulivyokwisha kumsikia Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi hivi juzi kwamba tayari ripoti ya mshauri muelekezi imeshafika serikalini na sasa hivi serikali zote mbili zinajadili ripoti hii. Lakini baadaye kwa upande wa Zanzibar maamuzi yoyote ambayo yatakayofanyika katika Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakuwa ni wadau wakubwa kuweza kutoa maoni na msimamo wa Zanzibar.

convert

4. Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu. Suala hili mpaka sasa hivi linakwenda vizuri kwa sababu tayari kuna mashirikiano makubwa katika wizara zetu mbili ya uvuvi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Zanzibar kwa kweli maendeleo yanakwenda vizuri na tunategemea baada ya kikao cha Febuari pengine na suala hili halitarudia tena katika kero za Muungamo litakuwa limekamilika.

5. Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje. Hili bado mazungumzo yanaendelea na tunategemea katika kikao chetu cha Febuari. Hili litakuwa halijamalizika lakini kuna taratibu kwa sababu kuna mambo mengine itabidi lazima tuyaingize katika Sheria. Sasa hili tunategemea tuliwekee utaratibu wa kisheria hasa ili huko mbele lisije kutuletea matatizo.

6. Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano. Hii tayari katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano Tanzania ameshatoa toleo na sasa hivi liko katika mchakato wa kufanyiwa kazi. Kama nilivyosema na hili vile vile linahitaji utaratibu wa kisheria ili tuliweke katika utaratibu mzuri lisiwe suala la kubahatisha wala mtu kujifikiria yeye mwenyewe.

7. Utekelezaji wa "*Merchant Shipping Act*" katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uwezo wa Zanzibar kujiunga na "*IMO*". Hili nadhani matunda yake tumeanza kuyaona kwa sababu mswada ambao umeletwa hapa na Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ni moja katika mafanikio ya hivyo vikao vyetu ya Kero za Muungano

8. i) Mgawanyo wa mapato yatokanayo na;
   - Misaada kutoka nje
   - Misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IMF*
   - Faida ya Benki Kuu

   ii) Uwezo wa SMZ kukopa ndani na nje ya Nchi

   iii) Hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizokuwa katika Sarafu ya Afrika Mashariki. Hili bado linaendelea na kimsingi mchakato wake hili utachukua muda mrefu kwa sababu chanzo chote cha hizo kero kwa kweli iko katika maeneo haya. Kwa hiyo hili tunalifanyia kazi kwa makini zaidi ili kuhakikisha kwamba yale maamuzi ambayo yatakuja kutolewa mwishoni basi yawe ni maamuzi yatakayoweza kuifaidisha pande zote mbili za Muungano.

9. Malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili. Hili bado linaendelea na kuna kamati ambayo katika kikao chetu cha Bwawani Mhe. Makamo wa Rais aliunda Tume ya watu 8 wanne kutoka Zanzibar na wanne kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya wafanyabiashara kupitia *TRA*.

10. Kutafutwa uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya kugharamia mpango mkuu wa umwagiliaji Zanzibar. Suala hili tayari Wizara ya Kilimo wameshakaa na wenzao Tanzania Bara na tayari mchakato unaendelea uzuri. Kwa hivyo, utaratibu ambao uliokubaliwa sasa hivi kwamba miradi yote inayohusiana na kilimo itakayoombwa kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa misaada ya nje basi ya *package* ya Zanzibar itakuwa ni *Included*. Kwa hiyo suala hili vile vile tunashukuru huenda katika kikoa chetu kitakachokuja likatoka katika hizi kero za Muungano.

(a) Mhe. Mwenyekiti, napenda kulijuilisha Baraza hili Tukufu kwamba mpaka sasa suali la Utekelezaji wa *"Merchant Shipping Act"* kama nilivyoeleza katika Jamhuri ya Muungano na uwezo wa Zanzibar kujiunga na "*IMO*" pamoja na suala la sheriza za Haki za Binaadamu haya ni masuala ambayo tunatagemea tutayafuta kabisa katika kikao kijacho na yatabakia hayo manane.

Lakini tunategema pengine katika kikao hiki kitakachokuja basi nadhani karibu kuna mawili tunategemea basi pengine yatabakia masuala 6.

Sasa kama yatajitokeza mengine tutayaingiza katika kero lakini tunashukuru kwamba vikao vyetu sasa vinakwenda vizuri na kuna mafanikio makubwa ambayo yameanza kupatikana.l

(b) Kwa kuwa serikali zote mbili zina nia njema kabisa ya kutatua kero hizo, tunaahidi kwamba haitachukua muda mrefu zitapatiwa ufumbuzi. Aidha, ni juzi tu tarehe 19/1/2009 kulikuwa na kikao cha Makatibu Wakuu wa pande zote mbili kujadili masuala haya na ripoti yao wataileta katika kikao chetu ambacho kitakachofanyika mwishoni mwa mwezi wa Febuari. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mhe. Waziri jinsi ambavyo alikuwa anatutajia orodha za kero ambazo zinashughulikiwa katika kamati ya pamoja ya Mhe. Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu kwa sasa hivi ni Makamo wa Rais.

Kuna suala nyeti sana ambao ni sugu katika masuala ya Muungano sijamsikia akilitaja hata mara moja. Mimi nilikuwa nataka nijue tu hili, *status* yake iko vipi na ni suala linalohusiana na Tume ya Pamoja na Fedha ambayo ripoti yake imeshakabidhiwa katika serikali zote mbili toka mwezi wa Agosti mwaka 2006 na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa pande zote mbili tumekuwa tukilihoji ndani ya Baraza hili na jibu tunalopewa ni kwamba bado serikali zinaendelea kutafakari. Nilikuwa naomba nipate maelezo juu ya suala hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, suala la Tume ya Fedha ya Pamoja suala hili ni kweli kuna ripoti ambazo zimewasilishwa katika serikali zetu mbili. Lakini kama nilivyoeleza kwamba katika mchakato wa masuala ambayo yaliyokuwa yanajadiliwa katika kero za Muungano moja ni katika masuala ambayo hii Tume ya Fedha ya Pamoja ndio iliyokuwa inayafanyia kazi. Kwa kuwa kulikuwa na mambo mengi ambayo kama nilivyoeleza katika kifungu cha 8 kuna suala la mgawanyo wa mapato linatokana na misaada ya nje misamaha ya mikopo ya fedha na zaida ya Benki kuu hizo SMZ kukopa nje ya nchi, hisa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki. Sasa baadhi ya mambo bado tulikuwa yana mgongano.

Kwanza tuhakikishe kwamba hizi kero ambazo tunazizungumza basi ziwe zinakwenda sambamba na hii ripoti ya hii Tume ya Fedha ya Pamoja. Kwa hiyo, ndio maana tukasema kwamba suala hili la Tume ya Fedha ya Pamoja kwa sababu kwanza kuna hata hili suala lake la Utawala kuna muda wake ulikwisha. Kwa hivyo, kulikuwa kunahitaji kuingizwa watendaji wapya ambao watakaoweza kushughulikia masuala haya.

Kwa hivyo, tunategemea Waheshimiwa pengine katika kikoa chetu cha Aprili tunategemea tukaja na ripoti nzuri sana ambayo itayoainisha hii taarifa ya Tume ya Fedha ya pamoja. Kwa sababu tukisema kwamba tutoe ile ripoti ya mwanzo lakini huku kuna mambo mengine bado hatujakubaliana sasa tunahisi kwamba tutakuja kuwa tunafanyakazi kinyume nyume. Sasa Waheshimiwa tuaminini na Mhe. Waziri Kiongozi kila siku ananisukuma kwamba hebu fuatilia hili kwa sababu hatusubiri mpaka kwenye vikao. Mambo tunayafuatilia ili kwenye vikao iwe tumefikia pahala pazuri. Kwa hiyo, tunajitahidi sana tunategemea pengine katika kikao cha April tukija tunaweza kuwa na ripoti nzuri zaidi ambayo Waheshimiwa tunategemea kuwa na nyinyi mtairidhia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa zaida kuanzia pale Mhe. Waziri Afisi ya Waziri Kiongozi alipomalizia.

Waheshimiwa Wajumbe ni kweli katika kila Bajeti ya Afisi ya Waziri Kiongozi na Wizara ya Fedha Wajumbe wamekuwa wakiuliza sana kuhusu Tume ya pamoja ya Fedha na ripoti iliwasilishwa serikalini. Kauli yangu nimekuwa nikisema kuwa jambo hili ni kubwa na linahusu maslahi ya Zanzibar. Masuala ambayo yanahusu masuala ya watu si vizuri kuyafanyia mzaha hivi na haraka haraka. Ripoti ile ina mambo mengi kweli na mambo mengine kusema kweli ukiyapitia haraka haraka yanakanganya kweli.

Waheshimiwa Wajumbe mtakubaliana na mimi sijui Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kama alikuwepo. Ripoti ile Waheshimiwa Wajumbe Waziri wa Fedha na watu wake tayari wameshaileta ikajadiliwa hapa na katika mjadala huo sasa Waheshimiwa Wajumbe sijui kama siku hiyo alikuwepo Mhe. Fatma Abdulhabib kama siku hiyo alikuwepo walitoa baadhi ya maoni yao. Sasa ni jukumu la serikali yale maoni nyinyi mliyotupa pamoja na maoni ya serikali tuyaweke pamoja ili sasa tufanye uamuzi. Mtakumbuka tulipokuwa tunazungumza juzi tulipokuwa kwenye semina ya Soko la Pamoja.

Waheshimiwa Wajumbe nyinyi mlisema masuala yanayohusu Taifa yafanyiwe kazi kwa umakini mkubwa sana, na kwa maana hiyo basi mara nyingi mimi nasema kama kuna hoja inatolewa na Wajumbe na hoja hiyo ina mantiki basi serikali inapaswa kuwa makini sana katika kulifanyia kazi suala hilo.

Sasa nasema jambo hili ni kubwa lakini tukishafanya maamuzi ya haraka haraka tukikosea ni heri tuchelewe lakini tunachelewa kwa sababu kwamba ripoti tuipitie mpaka. Maana yake tufikie mahala tuelewane kama lilivyo suala la Mafuta. Tumesema maamuzi tutayafanya lakini si vizuri tukasema kwamba kesho asubuhi tunatoa maamuzi mpaka tufike mahali serikali na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe mnasema kwamba huu sasa ndio msimamo wetu na haya ndio maoni yetu na sidhani kama tumefikia mahali hapo.

Jambo hili ni kubwa tuna hamu na kama nilivyokuwa nikisema kwamba katika ripoti ile kuna jambo moja limependekezwa *formula* ya kugawanya mapato ni asilimia 4. Tunasema ile ya kwanza ya awali iliyopendekezwa na Shirika la Fedha Duniani ile ilikuwa ni asilimia 4.5, itawezekanaje sasa kutoka asilimai 4.5 na kurudi.

Sasa ni jambo ambalo kusema kweli si vizuri kulifanyia haraka haraka tu hivi hivi tukae Waheshimiwa Wajumbe nyinyi mmeshaipitia ripoti hiyo mneshatoa maoni yenu na sisi kama serikali tuyazingatie maoni yenu na tuoanieshe na mawazo ya serikali halafu baadaye *inshaalla* tutajitahidi kadiri iwezekanavyo mwaka huu tuanze kufanya maamuzi hayo. Huu ndio ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa Mhe. Waziri Kiongozi katika kusaidia majibu mazuri amesema suala hili halihitaji haraka.

(a) Je, kiasi miaka 40 zinaweza kumalizika kero hizi.

(b) Katika mazungunzo haya Mhe. Mwenyekiti inaonekana kwamba hakuna. *priority* inayopewa katika mazungumzo. Hawaoni kwamba mazungumzo haya kuna *priority* zilizopangwa na *priority* ya kwanza ilikuwa ni ile Kero za Wafanyabiashara kutozwa ushuru mara mbili.

(c) Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba mfumo wa majadiliano ulioko sasa si mzuri kwa sababu unashirikisha watu wachache. Hawaoni kwamba kuna haja ya mfumo wa majadiliano ukawa mkubwa zaidi ukashirikisha watu ambao hawaoni haya katika majadiliano.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:**

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyomjua Mhe. Haji Faki Shaali ni mtu wa utani sana, maana yake anasema hii *speed* ambayo tunakwenda nayo labda kuwa kunavyofikiria kwamba hatutofika miaka 40.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sasa nataka nizungumze suala moja. Suala la kero za Muungano hazitokwisha. Kwa sababu Muungano ni sawa sawa na familia mnapoishi katika familia leo mtoto ataumwa na utampelekea hospitali. Lakini kesho litatokezea tatizo jengine.

Kwa hiyo, ina maana hizi kero mfumo mzuri ambao alianzisha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano huu ndio utakaoweza kutuwezesha kutatua hizi kero. Kwa sababu hizi kero zilijikusanya kwa muda mrefu kwa sababu kulikuwa hakuna vikao vya kujadili kero ilikuwa kila siku zinaongezea hakuna anayetatua.

Lakini kwa mfumo ambao tunakwenda nao sasa hivi Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani katika mambo 10 sasa hivi kuna mambo karibu manne tunategemea huenda katika kikao hiki tukayamaliza kabisa, yatabakia sita. Lakini sio kama yakibakia hayo yatakuwa yamemalizika tutakuwa tunasikiliza mijadala mbali mbali katika vikao vyetu mbali mbali.

Waheshimiwa ripoti za Wenyeviti wa Kamati sisi ndio wenyeviti wa Kamati pamoja na viongozi wa Kambi za Upinzani zile tunazikusanya ili kuweza kuangalia yale yaliotuhusu Zanzibar tunatatua sisi wenyewe. Yale ambayo yanahusu kero za Muungano tunakuja kuyaingiza tena. Kwa hivyo, ina maana

haya yatakuwa yanapungua na mengine yanaongezeka. Kwa hiyo, huu nadhani tumeshafanya marekebisho yale na tumeandaa mfumo mzuri wa utaratibu wa kuzungumza matatizo yetu sisi wenyewe.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunaendelea kwa kuwa huu Muungano utakuwa sio kama utaishia miaka 40 mbele utaendelea kudumu. Kwa hiyo, baada ya sisi na hao watakaokuja wajukuu bado vikao hivi vitakuwa vinaendelea na tutawaomba hao Maraisi baada ya Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete watakaokuja basi mfumo huu na wao waje wauendeleze kwa sababu ni mfumo pekee ambao utakaoweza kutuendelea matatizo haya.

Kwa hivyo, miaka 40 Mhe. Haji Faki Shaali kwa haya tuliokuwa nayo sasa hivi tunaamini ndani ya mwaka kama yatakuwa ndio haya haya 10 tutakuwa tumeyamaliza. Lakini kama yatakuwa yamejitokeza vyengine basi hayo tutaendelea kuyadadisi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyosema haya masuala yalikuwa yamejikunja na yamejizonga. Kwa hivyo, hivi vikao vyetu Mhe. Mwenyekiti, havina haja ya kusema kuwa viwe na watu wengi sana kwa sababu ni hoja ambazo zinazoletwa na Waheshimiwa na tunazichukua na kwenda kuzifanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti, kule hatuoneani haya. Vile vikao sema haviwi a*live* lakini kama vinakuwa a*live* mngesema kwa kweli sasa hivi viongozi wetu wamefikia pahala kuwa wawazi na wakweli kiasi kama hiki nadhani haya matatizo yasingekuwa mbali. Vikao vyetu kwa kweli vinakwenda kwa uwazi zaidi na mimi nashukuru sasa hivi hata wenzetu Bara tofauti na huko nyuma.

Sasa hivi wanaonesha kuelewa kwa sababu hata baada ya vikao wanakaa wanaulizana kwani hili linatupa tabu nini? Labda hili lina tatizo la kisheria. Sasa haya ndio matatizo ya kisheria ndio yanakuja kuchukua muda kwa sababu itabidi mengine yaende Bungeni na mengine katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, mimi naamini tunakwenda vizuri na masuala haya ya mambo ya wafanyabishara katika *priority* ambayo tumeipa.

Ndio maana katika kikao chetu cha Bwawani tukaamua sasa tuunde Tume ya watu 8 ambao wao itakuwa wanakwenda moja kwa moja kuangalia masuala ya wafanya biashara na kesho kutwa nafikiri mmesikia kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar atakuwa na kikao cha mwanzo kabisa cha ile *Bussiness council*. Kwa hivyo, miongoni mwa vikao hivi yataweza vile vile kusaidiwa na mambo mengine ambayo katika hizi kero kuweza kutatuliwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa mimi naomba tuwe wastahamilivu mambo yanakwenda vizuri. Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa masuala ya Muungano ni masuala nyeti na kwa kuwa hadi sasa Mhe. Waziri kakiri kwamba hakuna suala ambalo limefanyiwa utatuzi sahihi na kwa kuwa hadi hadi sasa wameunda tume mbili, kwanza Tume ya Fedha na Tume ya kushughulikia masuala ya Biashara.

(a) Mhe. Mwenyekiti, hadi tukimaliza kero hizo serikali itakuwa imemaliza kero ngapi ?.

(b) Kwa kuwa Tume hizi zina gharama kuwategemea kwa kutumia gharama kiasi gani na je, kuwa na mfuko maalum wa kushughilikia kero au ni fedha za walipa kodi ?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakunisikiliza vizuri nilipokuwa nikijibu suala la msingi kwamba anasema mpaka sasa hivi anasema hakuna kero ambazo zimepatiwa ufumbuzi. Nimezungumza kuwa kuwa kero mbili ambazo ndizo zimeshapatiwa ufumbuzi suala la Tume za Haki za Binadamu.

Huu mswada ambao tuliokuwa tumeupitisha jana ilikuwa ni miongoni mwa haya mafanikio ya hizo kero za Muungano. Sasa kama hivi tulivyoona kupitia vikao hivi tayari sasa hivi imesharuhusiwa na kujiunga na I*MO*. Kwa hivyo, mimi nafikiri matunda yameanza kupatikana.

Lakini vile vile ameeleza kwamba mpaka sasa hivi ni tume ngapi ambao zilizoundwa. Mhe. Mwenyekiti, katika vikao vya majadiliano, sio mkeshajadiliana lile suala litakuwa limekwisha mkeshajadiliana itakuwa pale pale mnawapa watu kazi kwa ajili ya kwenda kufatilia na hizi Tume sio labda wanatafutwa watu wa nje au watu kutoka sehemu gani, ndio hao hao watendaji katika hizo taasisi ambao zina kero zenyewe.

Kwa sababu kama masuala ya *TRA* ina manaa watatoka watu kutoka *TRA* na Wizara ya Fedha Zanzibar na sehemu mbali mbali pamoja na mwanasheria ili kwenda kuangalia yele matatizo. Kwa hiyo, ni sehemu ya kazi zao kwa sababu watendaji wetu wa serikali ni sehemu zao za kazi hizo hizo.

Kwa hivyo, sio kama tume hizi labda zitaleta tabu kwa sababu mafanikio ya kazi hizi mkeshafanya vikao maamuzi mlioyafanya mnakwenda kuyafanya na mnawatuma watu kuyafanyia kazi baadaye wanakuleteeni ripoti na halafu mkeshasaini lile suala linakuwa bado utekelezaji wake kwao unakwenda vizuri. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Mwenyekiti, suala hili Waheshimiwa wasiwe na wasi wasi sana.

Suala la Fedha, hizi zinazotumika za serikali ni kodi za wananchi na hata sisi tunazolipwa na Baraza la Wawakilishi ni kodi za wananchi. Kwa hiyo, ni moja katika matumizi ya fedha za serikali na ndio manaa tunahimiza kwamba tuweze kusimamia vizuri kodi na tuweze kukusanya vizuri ili hizi kazi zote za serikali ziweze kwenda vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 64**

**Hifadhi ya *Fire Hydrants.***

**Mhe. Anaclet Thobias Makungila -** Aliuliza:
Uchakavu na uchache wa visima vya kuchukulia maji ambavyo vingi kati ya hivyo vimeng'olewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara au ujenzi wa nyumba za kuishi, na ujenzi holela wa nyumba kama vile Tomondo unakuwa ni kikwazo kwa magari ya Zimamoto kufika kwa urahisi sehemu ya ajali ya moto pindipo inapotokea.

Je, Kikosi cha Zimamoto kinashirikiana vipi na taasisi nyengine juu ya kuweka miundo mbinu itakayorekebisha hali hii ?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ -** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake
Nam. 64 kama ifuatavyo:-

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar huwa kinawasiliana mara kwa mara na Taasisi nyengine za Serikali na za watu binafsi kwa kueleweshana umuhimu wa visima vya kuchukulia maji magari ya Zimamoto.

Kikosi kimekwisha kuiandikia Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati juu ya kuweka vifaa hivyo kwa zile sehemu ambazo havijawekwa hususan katika mradi unaoendelea hivi sasa wa kusambaza maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Aidha, kikosi cha Zimamoto na uokozi kimeingiza Wajumbe wake kwenye Kamati ya Ramani za Majengo Nchini yakiwemo Mahoteli na Majengo ya Biashara. Kamati hii huwa inazipitia ramani mbali mbali zinazowasilishwa kwa ajili ya kupata uhalali wa ujenzi unaokusudiwa. Miongoni mwa matukio yanayoangaliwa kwa kina katika ramani hizo ni masuala ya usalama wa majanga ya moto; na pia kutolewa maelezo ya njia za kupambana na majanga hayo.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, suala la uchakavu na uchache wa visima vya kuchukulia maji ni muhimu sana likaangaliwa hasa kutokana na majanga yanayojitokeza. Mwenyezi Mungu atujaalie yasitokee lakini hilo ni sehemu za kazi zao, basi likaimarishwa ili kuondoa kabisa tatizo hilo kwa kushirikiana na Wizara husika ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, toka asili na enzi katika nchi yetu tuna mfereji wa wima pale mtaa wa Mfereji wa Wima jina limesibu ndio hilo hilo mpaka leo. Lakini mfereji ule zamani ulikuwa unatumiwa sana na wanajeshi wanakuja kuchota wanaondoka na magari mengine ya zimamoto. Kwa muda mrefu pameachwa na pamesahaulika hata mfereji ulifikia wakati ukataka kuvunjwa na watu wasiojulikana lakini tuliudhibiti ili historia isife umebakia. Je, Mhe. Waziri, kwa kuwa mfereji upo katika pahala pa usalama na pazuri zaidi maana ni barabara ambayo haina mashaka kwa dharura yoyote inayotokea kwa magari yanayochukua maji. Ana utaratibu gani wa kuhakikisha yeye pamoja na wizara inayohusika kutembelea katika eneo lile na kulifnayia kazi ili mfereji ule ufanye kazi saa 24.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, ningependa kumfahamisha kwamba ule mfereji ni wa zamani na unajulikana na sidhani kama kuutembelea utaweza kuleta mabadiliko ya aina yoyote. Ni mfereji ambao umewekwa makusudi kwa kutoa maji. Kwa sasa hivi mradi huu wa maji unaofadhiliwa na Japan masuala hayo yameshaingizwa ndani ya ramani hiyo ambayo imekuwa ikisambazwa katika mji wetu. Kwa hivyo, mfereji wa wima pia umo katika masuala mazima ya maji ambayo kwa sasa hivi yamekuwa yakifanyiwa kazi.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kutokana na majibu yake je, ni vituo vingapi ambavyo vinafanya kazi kwa kuchukua maji hawa zimamoto hivi sasa kati ya mji wa Unguja na miji mitatu ya Pemba. Ikiwa kuna nyongeza ni vituo vingapi vinatarajiwa kuongezwa katika kipindi cha mwaka mmoja ujao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa swali lake linataka takwimu basi angenipa muda nikaweza kulifuatilia.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi zaidi juu ya vituo hivi vinavyotumika na Kikosi cha Zimamoto kwa Miji Mikuu ya Pemba na Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mhe. Waziri ni

kwamba katika mradi huu tunaoendelea nao wa usambazaji maji masafi katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika wilaya zake mbili, Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi, zote zimezingatia kuweka vituo hivyo kwa maana ya *point* za *fire hydrants,* ili kikosi hicho kitakapohitaji kutumia maji kwa ajili ya shughuli zake za zimamoto zitakuwepo.

Kwa upande wa Miji Mikuu Pemba, mradi ambao tayari tumeshaweka saini wenye thamani ya shilingi bilioni 70 na kuendelea ambao utahuisha usambazaji maji safi na salama katika Miji Mikuu yote mitatu ya Pemba, kwa maana matangi, visima na mabomba ya kusambazia maji. Tunategemea mradi huo utekelezaji wake kuanza Machi mwaka huu. Nao Benki ya Maendeleo ya Afrika ikishirikiana na Mamlaka ya Maji imezingatia kwenye Miji Mikuu yote mitatu ya Pemba kuweka vituo hivyo vya kuchukulia Kikosi cha Zimamoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea mradi huu wa mjini nao tunategemea kuanza mwezi Machi na kukamilika mwaka huu mwishoni. Pia mradi wa usambazaji maji kwa upande wa Pemba utaanza mwaka huu na kukamilika mwaka 2012.

### Nam. 83
### Wafanyakazi wa Shirika la Bandari Kupatiwa Nyongeza ya Mishahara yao

**Mhe. Salmin Awadh Salmin -** Aliuliza:-

Seriakli katika bajeti ya mwaka 2007/2008 iliongeza mishahara kwa wafanyakazi wake. Kwa kuwa wafanyakazi wa Shirika la Bandari hawakuweza kupata nyongeza za mishahara kutokana na kutokuwepo chombo cha kuidhinisha malipo hayo yaani Bodi ya Wakurugenzi. Na kwa kuwa hivi sasa chombo hicho kipo na kimeshaanza kazi zake.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako kupitia Shirika la Bandari, tayari limeshawalipa wafanyakazi hao nyongeza za mishahara pamoja na ile nyongeza *(arrear)* ya nyuma ambayo kwa wakati ule hawakuweza kuipata kutokana na kutokuwepo kwa chombo husika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake Nam. 83 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika bajeti ya 2007/2008 wafanyakazi wote wa serikali waliongezwa mishahara isipokuwa wafanyakazi wa Shirika la Bandari hawakuweza kupata nyongeza za mishahara kutokana na kutokuwepo

chombo cha kuidhnisha malipo hayo kisheria, yaani Bodi ya Wakurugenzi. Hata hivyo, baada ya kuundwa chombo hicho (Bodi ya Wakurugenzi) hapo Julai, 2008 wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ilichukua hatua ya kufanya marekebisho ya mishahara ya wafanyakazi wa Shirika la Bandari kwa kuidhinishwa rasmi utekelezaji wa kutumia ngazi za mishahara za Mfumo wa Utumishi wa Shirika hilo hapo Septemba, 2008.

Utekelezaji wa maamuzi ya bodi umeanza na wafanyakazi wote wamelipwa malipo yao ya mwezi wa Agosti, 2008.

Kilichofanyika ni kuanza kutumia mfumo mpya wa malipo ambao kila mfanyakazi wa shirika hulipwa mshahara kulingana na nafasi yake ya kazi ambayo amepangiwa ndani ya shirika hilo kwa kuzingatia muda wa kazi, elimu na dhamana aliyopewa, kila mfanyakazi wa shirika hilo alipata nyongeza hizo.

Wizara kupitia Shirika la Bandari ilifanya hivyo kwa vile Mashirika ya Serikali yanatakiwa yawe na mifumo yao ya Utumishi pamoja na kutoa fursa ya kuwa na ngazi zao mishahara ambazo huidhinishwa na Bodi za Wakurugenzi nje ya mifumo ya mishahara ya serikali.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa hatua waliyoichukua. Lakini naomba niulize swali moja tu ambalo sikulipatia ufumbuzi zaidi. Suala la *arrear* za wafanyakazi hawa tokea pale serikali ilipokatisha mishahara. Je, limezingatiwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine suala la *arrear* vile vile limeingizwa katika masuala haya.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza niwapongeze kwa kuwaingizia nyongeza za mishahara. Lakini kazi ya mawasiliano ni ngumu na mara nyingi baada ya mishahara huwa wanahitaji *overtime* na kwa muda mrefu wanailalamikia. Hii *overtime* ya wafanyakazi hao tayari wanapata au bado kuna ugumu wa kupata *overtime* katika wizara yake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, bado wizara yangu haijapokea malalamiko hayo, lakini kama kuna tetesi hizo basi wizara yangu itazifanyia kazi ili kuona kwamba malalamiko hayo tunayashughulikia mara moja.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu hayo kwa swali la Mhe. Ame Mati Wadi. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa Shirika la Bandari wanalipwa *overtime* zao kama kawaida, tena ni moja ya taasisi ambazo zinalipwa vizuri *overtime* zao. Hakuna mashaka yoyote na mishahara yao pia ni mizuri.

**Nam. 35**

**Kazi ya Uchoraji wa Nambari za Vyombo vya Moto**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu -** Aliuliza:-

Utaratibu uliozoeleka tangu zamani ni kuwa mwenye chombo au mmiliki wa chombo cha moto hufanya usajili wa chombo chake Baraza la Manispaa, lakini nambari za chombo huandikwa au huchorwa na mtu yeyote mchoraji mwenye sifa na ujuzi na haijatokea nambari hizo kukataliwa na polisi *(traffic)* barabarani.

(a) Nini sababu za Wizara ya Fedha kulazimisha nambari zote za magari na vyombo vya moto zichorwe au ziandikwe na mtu mmoja.

(b) Wizara yako ina uhusiano gani na maslahi gani ya kibiashara na mtu huyo. Kama upo uhusiano wowote serikali inapata maslahi gani kwa kazi hiyo ya usajili wa nambari za magari na vyombo vya moto.

(c) Kama serikali haina maslahi yoyote katika kazi hiyo, kwa nini wizara yako iwachagulie wenye vyombo vya moto kampuni/mtu wa kuwafanyia au kuwaandikia vyombo vyao badala ya wenye vyombo na wamiliki wa vyombo hivyo kuchagua wachoraji ama waandishi wanaowataka wenyewe.

(d) Ni chombo gani cha serikali kinachopaswa kusimamia usajili huo – ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi au Wizara ya Fedha, kama Wizara ya Fedha ni kwa misingi gani.

(e) Na kama serikali ilikuwa na nia kweli ya kupata mapato yasiyotiliwa shaka na wasi wasi. Kwa nini kazi ya uchoraji wa nambari za magari au usajili mpya wa magari isiachiwe taasisi husika yaani Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kumtumia mchoraji wao mkuu au mwandishi wa magari anayehusika.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye vifungu (a), (b), (c), (d) na (e) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, sababu iliyoifanya Wizara ya Fedha na Uchumi kuamua nambari zote za vyombo vya moto ziandikwe na kampuni moja ni kama zifuatavyo:-

i) Kuweza kuwa na udhibiti wa utoaji wa nambari hizo ili kutokutoa mwanya wa upotevu wa mapato ya serikali kama ilivyokuwa hapo mwanzo.
ii) Kuziweka nambari za usajili wa vyombo vya moto katika kiwango cha kimataifa kama ilivyo katika nchi nyengine duniani ambapo nchi zote za *SADC* pia zimekubaliana kuwa na mfumo wa nambari wa aina moja.
iii) Kuwa na udhibiti wa usalama wa nambari za vyombo vya moto kwa kuweka alama za usalama *(Security Features).*
iv) Suala hili lilikubaliwa na kupitishwa kwenye Baraza hili Tukufu katika kikao chake cha kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/2009.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar katika suala zima la usajili wa vyombo vya moto haina maslahi yoyote ya kibiashara na kampuni inayotoa sahani za nambari *(plate number),* kwani Wizara ya Fedha na Uchumi huwa haifanyi biashara na kampuni yoyote zaidi ya kuhitaji huduma mbali mbali kutoka kwa makampuni hayo ambapo Sheria za Manunuzi ya Serikali *(Procurement Act)* ya Mwaka 2005 zinafuatwa, ambapo taratibu zilifuatwa kwa kutangaza tenda.

Katika tenda hiyo kama nilivyozungumza jana jumla ya kampuni tatu (ambazo ni *Masasi Signs Company* ya Dar es Salaam, *Budda Auto Party* ya Zanzibar na *Link Way Zanzibar Ltd)* zilinunua *Tender Document* yenye thamani ya shilingi laki moja na kampuni mbili zilirudisha tenda hizo. Baada ya kufanyiwa tathmini ya tenda hizi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kampuni inayotengeneza nambari hivi sasa ndio iliyoshinda.

(c) Kuhusu maslahi ambayo serikali inapata kutokana na usajili wa nambari za magari na vyombo vya moto. Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba katika zoezi zima la utoaji wa

nambari serikali huwa inatoza kodi kama ilivyo kwa biashara nyengine yoyote inayofanywa na kampuni zilizosajiliwa hapa Zanzibar na kufanya biashara.

Kama nilivyosema katika kujibu swali la kifungu cha (a) kwamba serikali haina maslahi yoyote ya kibiashara katika suala zima la usajili wa vyombo vya moto. Sababu zilizoifanya serikali kutoa uamuzi wa kutangaza tenda na kuipa kampuni moja iliyoshinda ni kama nilivyozieleza katika kifungu (a).

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumtoa wasiwasi Mhe. Mwakilishi pamoja na wajumbe wote kwa jumla kwamba taratibu zote za zabuni kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Serikali ya Mwaka 2005 zilifuatwa hadi kupatikana kampuni iliyoshinda. Hata hivyo, mwanya wa kampuni zaidi ya moja kushirikiana katika kuifanya kazi hiyo ulikuwepo lakini hakukuwa na kampuni za namna hiyo zilizojitokeza.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri, huyu mkandarasi aliyepewa kazi hii ya kutengeneza *plate number* kwa jina la *Budda Auto Works* ali-*invest* kiasi gani katika mtambo na analipwa kiasi gani kwa kila plate, analipwa na nani, na hadi sasa ameshalipwa kiasi gani.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba huyu mkandarasi aliyeshinda tenda hii, sio lazima aliyeshinda kwanza niseme kwa ujumla hii kazi yenyewe inahitaji mtu uwe na *resources* za kutosha. Hii kazi sio ndogo kama tunavyoifikiria, hii kazi ni kubwa na nzito. Kama nilivyozungumza hata jana kwamba baada ya vigezo vile vilivyowekwa huyu ndio aliyeshinda.

Baada ya kushinda yeye mwenyewe ilibidi akakope mkopo benki siwezi kusema kiasi gani. Kwa sababu kama nilivyosema hizo *resource* zinazohitajika ni kubwa na nitatoa mfano kama ulivyouliza swali. Ilibidi anunue mashine tatu kwa sababu ile kazi inakwenda sambamba, kuna mashine moja inaitwa *hot filling machine* na mashine mbili nyengine. Kila mashine inagharimu dola 70,000 lazima ufikiri kwamba hii kazi sio ndogo.

Sasa hawezi kuwa na mashine moja tu kwa hiyo kanunua mashine mbili ambazo ndio zinaandika vile vibati. Kwa hivyo, kila kitu ni cha kileo na *very sophisticated.* Suala mkataba kiasi gani na kishalipwa kiasi gani. Suala hilo kidogo naona mheshimiwa bora tukutane nikupatie.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uandishi huu ni mzuri na gari zinaonekana za aina moja. Je, kuna mpango gani wa serikali kwa gari za SMZ nazo kuziingiza katika mpango huu. Je, mpango huu wa SMZ unaoana na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuziandika namna hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, kweli kama nilivyozungumza kwamba tunajaribu sote nchi zilizokuwepo kwenye *SADC* kuwa na mfumo mmoja. Naamini hata gari za serikali nazo tuna aim kwenye mfumo huo. Kwa sasa gari zetu za serikali hazijaanza bado lakini tunaelekea kwenye mfumo mzuri wa kuwa na vibati. Kwa sababu usipoangalia huko mbele hata majambazi wanaweza wakachukua kibati chochote wakaandika SMZ wakachukua gari wakenda wakafanya ujambazi. Sasa tunataka tuchukue hadhari kwamba askari anapoikamata aone kweli hiki ni kibati cha gari ya serikali. Kwa hivyo, nakubaliana na wewe kwamba tutaandaa utaratibu maalum kwa gari za serikali.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kimsingi mimi nimemfahamu sana Mhe. Waziri na majibu yake na nimemuelewa sana na sipingani hata kidogo na utaratibu uliowekwa. Lakini suala langu ni kwamba utaratibu huu unasababisha magari mengi kurundikana pale ilipo ofisi ya *ZRB* ambapo ndio *highway* ya Zanzibar kutoka *Airport* kuja mjini. Je, haoni kwamba pana umuhimu wa kutafuta eneo jengine ambapo magari yanaweza yakawa yanasubiri huduma kuliko pale ambapo ndio *highway* panafanya udhia mkubwa kwa watu wengine wanaopita.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kwanza lazima nimpongeze Mhe. Said Ali Mbarouk kwa *observation* yake na nimshukuru sana kwa ushauri wake. Nafikiri ni suala lililo wazi kwamba kweli pale pana msongoamano na kidogo panasababisha magari yasiende vizuri. Nafikiri hilo tutalichukua. Mimi leo mwenyewe nilkuwa pale ofisini nilikwenda kuangalia ndani kule hata ile hali ya ofisi na walipa kodi ilivyo na tukashauriana vilivyo. Kwa hivyo, hilo la barabarani tumelisikia na tutalifanyia kazi.

**Nam. 92**
**Kukatika kwa Umeme Pemba**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin –** Aliuliza:-

Hivi sasa kumekuwa na tatizo la kukatika kwa umeme kila mara katika kisiwa cha Pemba, hii ni kutokana na uchakavu wa mashine ziliopo. Kwa kuwa mradi wa kununua mashine mbili (2) mpya zenye uwezo wa kuzalisha umeme wa 2

MW kila moja umekwama kutokana na fedha zilizotengwa, zilikuwa nusu tu ya fedha zinazohitajika. Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba fedha zaidi zinapatikana ili kuondosha tatizo hilo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa gharama za mradi wa upelekaji wa umeme kutoka Tanga hadi Pemba, serikali imekubaliana na Washirika wa Maendeleo wa Mradi huu, kuacha mpango wa ununuzi wa mashine mbili mpya za kuzalisha umeme na badala yake kutumia fedha zilizokusudiwa kununuliwa mashine hizo ziongezwe katika mradi wa kuweka waya wa baharini.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuhakikisha kwamba hivi sasa tunaamini mwelekeo wa kupatikana umeme wa uhakika Pemba upo mbioni na Mwenyezi Mungu akitujaalia Ilani ya Chama cha Mapinduzi itatekelezeka.

Lakini pamoja na hayo niulize swali.

(a) Lengo la mradi huu wa umeme kutoka Tanga Pangani hadi Pemba utakamilika lini.

(b) Kwa kuwa kuna gharama zimeongezeka kwa kiasi fulani. Je, gharama hiyo ni kiasi gani na atazitoa nani. Sababu ya kuuliza hivyo ni kwamba kuna serikali na mfadhili.

(c) Huu waya una uwezo wa *megawatt* ngapi, ili wananchi waelewe kutokana na umadhubuti wa kazi zao.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishari na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu akipenda mradi huu tunategemea mwezi wa Disemba mwaka huu utakuwa unafanya kazi. Kwa maana wananchi wa kisiwa cha Pemba watakuwa wanapata umeme kutokana na waya huu wa umeme wa baharini unaotoka Tanga. Hivi sasa kazi ya utengenezaji wa waya inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, gharama za mradi huu Serikali ya Norway ilitenga jumla ya dola 52 milioni. Kwa bahati mbaya gharama zikaongezeka hadi kufikia dola 75 milioni. Serikali ya Norway ikasema haina fedha ya kuongezea. Kwa maana

walitwambia mkitaka mradi huu uendelee fedha za ziada ambazo 22.5 milioni za dola zitafutwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bahati nzuri na namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, baada ya kutajiwa fedha hizo wizara tuliteteruka lakini yeye hakuteteruka akasema zitatafutwa na zitapatikana. Kwa hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikajitolea kutoa dola milioni 15 kati ya hizo 22.5 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar kwamba tayari awamu ya mwanzo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni dola milioni 5 zimeshatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikubali kutoa dola 7.5 milioni na tayari 2.5 milioni zimeshatolewa. Ulipaji kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unaendelea vizuri na Serikali ya Norway nayo inaendelea kulipa kwa muda huo uliopangwa. Kwa hivyo, malipo nayo yanaendelea vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, waya huu utakuwa na uwezo wa megawatt 20. Hivi sasa matumizi kisiwani Pemba ni 4.6 *megawatt*. Kwa hivyo waya huu utawasaidia wananchi wa Pemba kwa miaka mingi ijayo na tunategemea kwamba tatizo hili la kukatika umeme kwa uchakavu wa vinu vyetu na ukosefu wa *IDO*, Mwenyezi Mungu akipenda ifikapo Disemba itakuwa historia. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Ali Salim:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, swali langu litapelekea kuniondolea utata uliomo ndani ya kichwa changu. Kwa sababu katika Baraza hili kwanza tuliambiwa pesa zile zilizozidi zitatolewa kwenye barabara za Kusini Pemba. Baadae tukaambiwa sasa hivi mfadhili kakubali kutoa yeye na barabara kaziweka pale pale, katika Baraza hili hili. Leo tunaambiwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndizo zilizotoa fedha hizi, naomba katika mambo haya matatu niambiwe la ukweli ni lipi?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, aliyozungumza Mhe. Moh'd Ali Salim ni sahihi kabisa, ni suala la msingi na ni haki kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kupata ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, lililotokea ni hili. Barabara zile za Kusini ambazo zilitengewa dola milioni 10, fedha zile zimetiwa kwenye mradi huu wa umeme. Lakini baada ya maamuzi ya kijasiri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuonesha imani ya kutaka mradi ule uendelee, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikakubali kuzitafuta hizo dola milioni 22.5 nilizowaambia, Serikali ya Norway ikasema hapana. Hizi fedha za barabara tutawatafutia sasa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hakuna lililoharibika. Dola milioni 10 zilitiwa kwenye mradi wa umeme na hilo halijabadilika, lakini Serikali ya Norway kutokana na maamuzi yaliyofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kijasiri, ndio ikasema hapana na hizi barabara tutahakikisha hamzikosi. Kwa hivyo, wao wamezitafuta zile dola milioni 10 na kuipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Naamini baada ya ufafanuzi huo, ule utata uliokuwepo kwenye kichwa cha Mhe. Moh’d Ali Salim, Mwakilishi wa wananchi katika Jimbo la Mkoani utakuwa umemalizika.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa heshima kubwa naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Mwenyekiti, sababu za umeme Pemba kukatika ovyo ovyo, moja ni uchakavu wa mashine zetu. Lakini suala la pili ni upungufu wa mara kwa mara wa IDO.

(a) Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri, kutokana na hali hii atakuwa tayari kushirikiana na Kamati ya *PAC*, kufanya *IDO investigation*, ili Wazanzibari waelewe kuna nini?

(b) Tumemsikia Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme amepewa likizo bila malipo kwa muda fulani. Kwa hivyo, ningeomba tuelewe kama ni Wazanzibari kulikuwa kuna sababu gani?

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haioni sababu ya kukataa kushirikiana na *PAC* kwa jambo lolote lile. Ni utaratibu na kilele cha uwazi na usimamizi wa demokrasia na fedha za watu. Kwa hivyo, *PAC* itakapohitaji suala lolote katika utaratibu wake wa utendaji wa kazi kwenye Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, basi tutawasaidia na ni wajibu wetu kufanya hivyo.

Lakini nitowe ufafanuzi wa masuala ya *IDO*. Mhe. Mwenyekiti, kisiwani Pemba Shirika la Umeme lina wateja wanaokaribia 13,000 hivi. Wanalipa milioni 100 hadi milioni 115 au milioni 120 inategemea na matumizi ya mwezi huo.

Mhe. Mwenyekiti, gharama za uzalishaji wa umeme kwa upande wa Pemba, mafuta yalipopanda bei ilifikia hadi bilioni 1.2. Shirika likawa linapata hasara kwa maana ya *subvention* ya karibu shilingi milioni 956. Si kazi nyepesi kwa shirika kutafuta shilingi milioni 900 kuzalisha umeme kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme halisaidiwi na serikali fedha hizo, Shirika la Umeme inabidi litafute lenyewe fedha hizo. Kwa hivyo, huwa tunategemea mwisho wa mwezi kukusanya fedha za wateja na kufanya malipo ya *IDO*. Mara nyengine kwa bahati mbaya hukosekana meli nakadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme …

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa hilo nadhani sio la msingi. Hilo la Meneja wa Shirika la Umeme si la msingi, tunazungumzia *leave without pay* ya mtu hapa Barazani, si suala la msingi.

**Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** Nilikuwa nataka kusema hivyo hivyo. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 68**

**Gharama za Kuwapeleka Wagonjwa nje ya Nchi kwa Matibabu**

**Mhe. Anaclet Thobias Makungila** - Aliuliza:-

(a) Je kuanzia mwaka 2007 hadi hivi sasa ni wagonjwa wangapi waliopelekwa matibabuni nchi za nje. Na kiasi gani cha fedha zilizotumika kwa ajili ya matibabu hayo.

(b) Ni magonjwa gani yanayoongoza kwa wagonjwa kupelekwa kutibiwa nje ya nchi.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 68 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wagonjwa waliopelekwa matibabu nchi za nje kuanzia mwaka 2007 hadi hivi sasa ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Watu wazima ni | = | 32 |
| Watoto waliopelekwa India | = | 26 |
| Watoto waliopelekwa Israel | = | 32 |
| Jumla: | = | 90 |

Fedha zilizotumika ni Tshs. 214,500,000/= (US$ 165,000.)

(b) Mhe. Mwenyekiti, magonjwa yanayoongoza kwa wagonjwa kusafirishwa nje ya nchi ni magonjwa ya moyo, na figo.

- Moyo = 58
- Figo = 6
- Maradhi mbali mbali = 26
- Maradhi haya ni kwa kipindi cha 2007 hadi hivi sasa.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa wagonjwa wanaopelekwa matibabu nje ya Zanzibar, yaani kuanzia Tanzania Bara na nchi za nje hulipwa kabla ya kuondoka.

a) Je, ni kigezo gani kinachotumika cha kulipa fedha hizo?

b) Kwa kuwa wagonjwa wanapopelekwa matibabu nje mpaka bodi ikae kitako na kuidhinisha ndio wagonjwa wapelekwe matibabuni nje. Je, kama Mhe. Mwakilishi alipopata matatizo ghafla kuanguka na gari akaumia, Mhe. Mwakanjuki alipelekwa nje. Je, bodi ilikaa kitako ikaidhinisha na kama haikukaa kitako je, fedha hizi zilitoka sehemu gani?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, nchi za nje kigezo huwa tunapeleka taarifa za yule mgonjwa, halafu wao wanatupa makisio, yale yanaitwa makisio ya mwanzo. Lakini malipo sahihi ni baada ya mgonjwa yule kufika kule nje kama ni India. Anatibiwa akisha kutibiwa ndio gharama zake zinaletwa hapa Zanzibar, halafu sisi ndio tunafanya malipo.

Kwa Tanzania Bara yule mgonjwa huwa tunamkisia, kama maradhi haya tukimpeleka *Ocean Road* itabidi gharama hizi, au tukimpeleka *KCMC* gharama hizi au Muhimbili ni gharama hizi. Kwa hivyo, tunamkatia kifungu tunampa fedha anaondoka nazo. Baadae anatakiwa alete risiti na mambo mengineo ya matibabu hayo.

Pia Mhe. Mjumbe aliuliza kwamba Je, bodi iliidhinisha kwa Mhe. Mwakanjuki alipoanguka na gari. Mhe. Mwakanjuki alipopata ajali Tanzania Bara, basi huko huko alipelekwa Afrika ya Kusini. Kwa hivyo, bodi hapa au wizara mimi sina taarifa yoyote, mambo yote yalimalizika huko huko Tanzania Bara na Serikali Kuu.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ndani ya Baraza hutokea wagonjwa ambao wanahitaji matibabu ya kwenda nje.

Je, Mhe. Waziri ni wagonjwa wangapi katika Baraza hili waliopelekwa matibabuni nje, ahsante?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na Tanzania ni mjumbe au tuseme tumo katika Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*), na (*WHO*) kuna *convention* ya *World Health* - Geneva inayomkataza daktari hata Waziri wa Afya kutoa siri za mgonjwa wazi wazi hadharani.

Kwa hivyo, nipate idhini ya wagonjwa hao wangapi niwataje, kwa sababu hapa wapo na idadi yao wanajijua, nikipewa idhini hiyo nitawataja mheshimiwa. Nipate ridhaa hiyo, kwa sababu nitawahesabu mmoja baada ya mwengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, suala sio majini ni wajumbe wangapi?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Ni wengi Mhe. Mwenyekiti, idadi kamili sinayo, itabidi niwatizame hivi nianze kuwahesabu mheshimiwa.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na kuyaweka wazi. Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine wananchi wanailaumu serikali kwa kutokupata maelezo sahihi kwa yale magonjwa ambayo yanahitaji kupelekwa nje.

Kwa mfano, magonjwa ya figo yana utaratibu wake namna gani mgonjwa anaweza akatibiwa huko katika hospitali ya India. Je, Mhe. Waziri suala hili nje ya sisi amewahi kulieleza ili wananchi wakae tayari kwamba ikitokea mgonjwa ana tatizo la figo, basi jamii inahitajika iweje, ili mgonjwa apate matibabu huko India?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ame Mati anataka kujua utaratibu wa kupelekwa mgonjwa wa figo.

Mhe. Mwenyekiti, inategemea kama mgonjwa ana matatizo ya mafigo yote mawili hayafanyikazi, anahitaji kupewa figo jipya, basi kwa utaratibu uliokuwepo hivi sasa ni kwamba mgonjwa yule inabidi atafute jamaa yake wa damu. Kwa sababu sasa hivi India kuna sheria iliyowekwa kwamba mtoaji figo anayempa mgonjwa ni lazima awe jamaa yake wa damu.

Pili, inabidi yule anayetoa figo tumpime afya yake na damu yake ilingane na mgonjwa yule. Ikipatikana mambo hayo yote mawili, basi tunayapeleka mambo yote ya mgonjwa pamoja na mambo yote ya yule anayetoa hiyo figo huko India na baadae wanatujibu na tunawafanyia safari ya kuwapeleka huko, tena utaratibu wa matibabu unaendelea.

**Nam. 98**
**Usafirishaji wa Wagonjwa Kwenda Nchi za Nje**

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** - Aliuliza:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa swali langu nambari 98(a) tayari Mhe. Waziri ameshalitolea ufafanuzi. Kwa hivyo, namwomba anijibu swali nambari 98(b)(c) na (d), na swali nambari 98(e) aliwache kwa sababu sio swali langu.

Serikali hulazimika kuwasafirisha baadhi ya wagonjwa na kuwapeleka nje ya nchi
kwa ajili ya matibabu zaidi, na huwapeleka nje ya nchi baadhi ya watu kwa ajili ya uchunguzi wa afya zao.

(a) Katika kipindi cha mwaka 2007 – 2008 ni wagonjwa wangapi wameweza kusafirishwa nchi za nje kwa ajili ya matibabu zaidi.
(b) Ni sifa zipi zinahitajika, ili mtu aweze kusafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya uchunguzi wa afya yake.
(c) Kwa kuwa wagonjwa waliokuwa wakipelekwa nchini India, walipelekwa katika hospitali maarufu ya Apollo. Je Mhe. Waziri, hivi sasa hupelekwa katika hospitali gani.
(d) Je, ni nchi zipi nyengine zinazopelekwa wagonjwa hawa.
(e) Kwa nini tusiwe na mfumo wa kuwatibu wagonjwa wetu nchini mwetu.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 98 lenye vifungu (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(b) Mhe. Mwenyekiti, sifa zinazohitajika ili mtu aweze kusafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya uchunguzi wa afya yake ni kama zifuatazo:-

- Ikiwa matibabu hayo hayapatikani nchini.
- Ikiwa mgonjwa afya yake itaimarika kwa matibabu hayo.
- Matibabu hayo yataweza kuokoa maisha yake.

(c) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu bado inaendelea kutumia hospitali za Apollo Delhi India na MIOT Chennai India. Hata hivyo tunaendelea kutafuta hospitali zaidi kwa kuzingatia upatikanaji wa huduma bora na nafuu.

(d) Mhe. Mwenyekiti, nchi nyengine tunayopeleka wagonjwa wetu ni Israel.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi kwamba hospitali ya MIOT ambayo wanapelekwa sasa hivi wagonjwa ni mbali sana na mji, na wagonjwa hupata tabu sana wanapohitaji huduma za Kibalozi inakuwa shida, ambapo Maofisa wa Kibalozi wa Tanzania huwapitia mara kwa mara na kuwasikiliza matatizo yao wale wagonjwa waliokuwepo Apollo, kinyume na ilivyo katika hospitali ile iliyoko sasa.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, nasema hospitali ya MIOT Chennai India iko mbali na pia hakuna fursa za Kibalozi. Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya MIOT, ni hospitali safi, nzuri na wala haiko mbali.

Unachukua ndege ya Emirate moja kwa moja kutoka Dar es Salaam, Dubai mpaka Chennai moja kwa moja wala sio mbali. Tena ni hospitali yenye sifa kwa maradhi ya mifupa, ukipasuka goti litatiwa utastaajabu. Kiuno kinawekwa sawa, mgongo unanyooshwa. Kwa duniani ni hospitali ya pekee hiyo ya MIOT Chennai na wenyewe wagonjwa waliofika pale wanajua na wanatambua. Hivyo, ni hospitali nzuri yenye kutibu vizuri kwa bei nafuu na hali ya juu kabisa. Balozi si anakuja kukutizama, lakini la umuhimu ni daktari na matibabu yenyewe. Balozi hatibu, anakuja kukusikiliza hali yako tu.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuniona na kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali hulazimika kusafirisha wananchi kwa kupelekwa nje kwa ajili ya matibabu.

Je, kuna kiwango maalum ambacho kimewekwa na kama si hivyo, basi ni sababu zipi zinazopelekea baadhi ya wananchi kuja kwenye televisheni kuomba misaada zaidi.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza sijafahamu. Hichi kiwango kakusudia kitu gani.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kiwango ambacho nimekusudia pengine kuna idadi maalum ya wagonjwa, kama labda huwa imeshafikia, kwa hiyo wale ambao wamezidi tena inabidi waje kwenye televisheni kuja kutafuta misaada ya kusafirishwa.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kiwango hakuna, isipokuwa uwezo. Sisi tunapeleka mgonjwa, mfano MIOT Chennai, anakwenda wa kwanza, anakwenda wa pili, anakwenda wa tatu na anakwenda wa nne. Halafu wao wanaleta gharama zao kwa mgonjwa mmoja baada ya

mwengine. Huyu kafanyiwa dawa hii na malipo yake gharama hii. Huyu kapewa hii na gharama zake hizi. Kwa hivyo, zinapokuja gharama zile kwa Mhe. Waziri wa Fedha, anatakiwa alipe kule hospitali ya Chennai.

Kwa hivyo, sisi Wizara ya Afya tunajua sasa hivi kwamba tunadaiwa kiasi hiki, kwa hivyo serikali inapolipa kule, sisi ndio tunakuwa na uwezo wa kupeleka wengine. Ikiwa bado deni lile halijalipwa, basi na sisi kidogo tunazuia zuia. Kwa hivyo, tunawapeleka tunalipa, halafu tunawapeleka tunalipa. Kwa hivyo, shughuli zinakwenda vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kigezo gani cha kuharakiza. Madaktari wangu wananiambia kwamba huyu aliyekuja ni hatari anaweza kufa, au huyu haraka aharakishwe na huyu kidogo asitesite. Kwa hivyo, tulipe na tuwapeleke kwa mpango maalum na mzuri sana.

Kwa hivyo, hatuna matatizo, tunawapeleka na tunalipa vizuri na tunawapeleka wagonjwa wanahudumiwa vizuri, shughuli inakwenda vizuri Mhe. Mwenyekiti, mpaka sasa hivi.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika kudhihirisha kwamba magonjwa mengi ambayo watu wanapelekwa nje kama moyo, figo na mengineyo na kwa kuwa serikali hutumia fedha nyingi sana ya kuwasafirisha wagonjwa hao na kuwahudumia.

Je, wizara ina mpango gani kupitia nchi rafiki, ambapo tunao wataalamu wa maradhi mbali mbali wakaja kuweka kambi yao hapa Zanzibar, ili kufanya uchunguzi wa maradhi hayo ya moyo na figo na kupata matibabu hapa hapa ili kunusuru fedha hizo.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman kauliza kwamba je, tuna utaratibu gani wa kupata wataalamu wa maradhi ya moyo na figo na pia shughuli hizi kufanyika hapa.

Mhe. Mwenyekiti, maradhi haya sio madogo, yanataka dhana, yanataka madaktari na dawa nzuri za kutosha. Kwa uwezo wetu na hali yetu ilivyo kwa maradhi haya ni vigumu kwa hivi sasa, lakini kwa hapo baadae tunaweza tukafanya mambo hayo. Lakini kwa sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, wazo lake ni zuri, lakini ni gumu kulitekeleza.

**Nam. 40**
**Matumizi ya Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu** – Aliuliza:-

Kwa kuwa sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu ya mwaka 1998 imepitishwa na kuanza kutumika rasmi pande zote za Muungano kuanzia June 2008.

(a) Je, makubaliano ya mgawanyo wa mapato ya uvuvi yatokanayo na Bahari Kuu yakoje, na hugaiwa kwa kila baada ya muda gani.

(b) Kwa kuwa sheria hiyo imepitishwa zamani (kipindi cha miaka kumi hadi sasa – 1998 – 2008), kwa nini utekelezwaji na kutumika kwake kumechukua muda mrefu kiasi hicho.

(c) Je Kanuni za kusimamia Mamlaka hiyo zinasimamiwa na upande gani na mamlaka ya Waziri wa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yakoje katika sheria hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Mazingira** – Alijibu:-
Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 40 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo mafupi juu ya Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu iliyopitishwa Bungeni mwaka 1998, kwamba hadi sasa bado haijaanza kutumika kwa sababu zifuatazo:-

(1) Sheria ya Mamlaka ilipitishwa 1998, ikiwa na mapungufu ya taratibu za uendeshaji wa chombo chenyewe kwa kuzingatia kuwa ni chombo cha Muungano na Uvuvi sio suala la Muungano. Hivyo haikuweza kutekelezeka.

(2) Mwaka 2007, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho ya msingi yafuatayo:-
    (a) Mgawanyo wa mapato kwa pande mbili za Muungano SMT na SMZ.
    (b) Uundwaji wa Kamati tendaji yenye Wajumbe sita (6) watatu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watatu (3) Serikali ya Jamhuri Muungano wa Tanzania itakayomsimamia Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na kumshauri Mhe. Waziri atakayesimamia Sheria hiyo.

(c) Kumtambua Waziri anayesimamia Uvuvi wa SMZ.

(d) Utayarishwaji wa Kanuni za sheria mama ya Mamlaka ambao bado haujakamilika, ndio sababu inayoifanya sheria hiyo, pamoja na kupitishwa kwa marekebisho niliyoyataja na Mhe. Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka saini kutotumika hadi sasa. Ni matarajio yetu kuwa kanuni hizo ambazo ndio ngao za utekelezaji wa sheria mama zitakamilika ndani ya muda mfupi ujao.

Kanuni za Mamlaka ya Sheria ya Bahari Kuu zinatayarishwa kwa pamoja kati ya wataalamu wa Uvuvi wa SMT na SMZ. Zitakapo kamilika Kanuni hizo zitakuwa chini ya sheria mama, ambayo msimamizi mkuu atakuwa Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Uvuvi kwa kushauriana na Waziri wa Uvuvi wa SMZ.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri je, kukubaliana na mgao kama huo na kuingizwa kwa mradi wa *MACEMP*, pamoja na Tanzania Bara. Haoni kwamba ni kulifanya hili jambo liwe la Muungano kinyemela.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa *MACEMP* ni tofauti kabisa na suala hili la Bahari Kuu. Ule mradi ni maalum ni wa muda maalum kabisa wala sio wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama umetiwa katika suala la Kimuungano.

Lakini suala hili la Bahari Kuu halitunyimi nafasi yetu ya ndani. Kwa sababu masuala ya uvuvi ya ndani bado kila mmoja atakuwa na lake.

Tanganyika watakuwa na leseni zao na sisi Zanzibar tutakuwa na leseni zetu. Isipokuwa hii mamlaka ya pamoja na Bahari Kuu ndio ambayo itakuwa na muundo wa Kimuungano, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

## HOJA YA KUTENGA KANDO KANUNI

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwa kuwa muda wetu wa Maswali na Majibu umemalizika kwa mujibu wa Kanuni ya 40 (2) naomba kunukuu.

Kanuni ya 40 (2) inayosema hivi:

> "Swali lolote halitaulizwa katika Baraza baada ya kupita muda saa moja na nusu tokea Baraza lilipoanza shughuli ya maswali na kama swali halikufikiwa, basi litajibiwa katika kikao kingine."

Kwa hivyo, kutokana kwa kwamba tunayo maswali mengi na muda wetu wa kuahirisha kikao chetu cha Baraza unakaribia. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuchukua fursa hii kueleza kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 150 cha Kanuni tuweze kuweka Kanuni kando ya 40 (2), ili tuendelee na Maswali na Majibu mpaka hapo yatakapomalizika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa niwahoji na wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri ya kutenga Kanuni kando yanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira**: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Omar Ali Jadi:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Lakini kabla ya kuuliza swali hilo naomba uniruhusu nitoe dibaji japo kidogo kwa kukusifu wewe.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwamba jana ulitoa upeo mkubwa sana hapa wakati ulipokuwa ukichangia mswada ambao upo mbele yetu hivi sasa. Mhe. Mwenyekiti, ulisema wakati Mtume Muhammad (*S.A.W*) kwa ajili ya kwenda Iraq aliwauliza maswali kama ni *interview*, kwa bahati nzuri wa mwisho ndiye aliyefaulu kwa sababu alitumia akili.

Kwa hivyo, ninakushukuru na wewe ulitumia busara na hekima kwa kutumia akili. Kwa sababu utaratibu wa Baraza mjumbe akeshauliza swali mara moja hapewi mara nyengine kabla ya mwengine kupewa. Lakini umetumia fursa hiyo kwa kumpa Mhe. Hija Hassan Hija nafasi. Ninakuombea kila la heri *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu bahari kuu itakuwa na mipaka yake na kutakuwa na utaratibu

maalum kwa upande wa Zanzibar na Dar-es-Salaam tunaweza kufika Lindi mpaka Mtwara. Je, kuna mfumo wa Afrika ya Mashariki na kwa upande wa kaskazini tumepakana na Kenya kwa maeneo ya bahari kuu. Je, katika mtandao huu wa bahari kuu Tanzania bila ya kushirikishwa Kenya, hatuoni baada ya Afrika Mashariki kujumuisha kufanya kazi zake, tutakuwa na kazi nyengine ya kubadilisha utaratibu huu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, shukurani kwa pongezi zake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hili naomba nilichukue na nitamjibu kwa maandishi.

**Nam. 50**
**Faida ya Uvuvi wa Majongoo Bahari**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Kny: Anactlet Thobias Makungila)** Aliuliza:-

(a) Uvunaji wa majongoo bahari unasaidia vipi katika suala la kukuza uchumi wa nchi na ni kiasi gani cha mapato yanayopatikana kutokana na usafirishaji wa majongoo bahari nje ya nchi.

(b) Majongoo bahari yanasafirishwa nchi gani na kwa matumizi gani.

**Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Mazingira –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Uvunaji wa majongoo ni mdogo sana kulinganisha na mazao mengine ya baharini. Hivyo usafirishaji wa majongoo hauna mchango mkubwa katika pato la Taifa.
(b) Usafirishaji wake hupelekwa Hong Kong China kwa ajili ya chakula.

**Nam. 25**
**Ujenzi wa Majengo ya Maonesho Zanzibar**

**Mhe. Ali Suleiman Ali –** Aliuliza:-

Mwezi wa Novemba 2008, yalifanyika Maonesho ya Biashara ya Afrika ya Mashariki, nchini Rwanda maarufu (Jua Kali), ambayo yalifunguliwa na Mhe.

Rais Paul Kagame, ambapo wafanya biashara wengi wa Zanzibar walishiriki katika maonesho hayo.

(a) Kwa kuwa Maonesho hayo yametakiwa kufanyika kila mwaka na kila nchi mwanachama anatakiwa kuwa mwenyeji. Je. Mhe. Waziri, wizara yako imejiandaa vipi na maonesho hayo pindi wakati wa kuwa mwenyeji utakapofika.

(b) Kwa kuwa tulikuwa na mabanda ya Maonesho huko Tunguu, lakini sasa eneo hilo linatarajiwa kujengwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Je, wizara ina mpango gani wa kutayarisha eneo jengine kwa ajili ya maonesho hayo.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji imeshafanya mazungumzo na Wizara ya Maji, Ujensi Nishati na Ardhi pamoja na Serikali ya Mkoa wa Kusini kutupatia eneo jengine kwa ajili ya maonyesho.

(b) Baada ya kupatiwa eneo jengine, wizara ina mpango wa kushirikiana na Bodi ya Biashara za Nje Tanzania. Hapa tunatumia fursa yetu Zanzibar ndani ya Bodi yenye sura ya muungano, ili kuwataka watujengee kiwanja cha maonesho. Kwa upande wetu ni kutafuta ardhi na *BET* itajenga kiwanja cha maonesho.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa nchi au biashara yoyote inatangazika kutokana na maonesho ya biashara mbali mbali. Kwa mfano, wenzetu Tanzania Bara wamejiwekea maonesho tofauti ya hasa yale ya Sabasaba, ambapo wananchi kutoka nchi mbali mbali za Afrika ya Mashariki na Kati huwa wanakuja pale kujionea na kuweza kupata masoko kwa ajili ya kueneza biashara zao.

Kwa kuwa maeneo ambayo Mhe. Waziri amesema kwamba wizara inafanya mpango kupata eneo hilo. Je, hivi sasa kuna maeneo kadhaa mazuri kabisa kwa mfano eneo la Dunga katikati ya nchi yetu, ambapo huduma muhimu zipo zikiwemo umeme, maji safi na barabara.

Vile vile kwenye maeneo ya Tunguu ambao ni mji mpya hivi sasa ambapo ni karibu zaidi kwa wananchi wetu kwa kufika na kuweza kujionea bidhaa tofauti na kupata mahitaji yao.

Hivyo, kati ya hayo maeneo mawili lipi analiona bora na kutoa wito kwa Mhe, Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi amfanyie haraka, ili maonesho yanayokuja tuyafanyie hapa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema kweli wizara imeomba eneo la Tunguu ambalo yeye amelipa sifa zote. Kwa hivyo, tunasubiri Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi wafanye mipango yao na wakati wanapokata maeneo ya aina hiyo, watupatie eneo kwa ajili hiyo *(Makofi).*

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Maonesho ya Kibiashara ni maonesho ambayo anatakiwa yule mfanyabiashara aoneshe bidhaa yake kama inavyoweza kuuzika kwenye masoko mengine yote katika nchi nyengine.

Ninapenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba wizara imejitayarisha vipi na kuwapatia ujuzi wafanyabiashara wa Zanzibar kuhusu *packing*, kwani bidhaa zetu nyingi zinashindwa kuingia katika soko kutokana na ubovu wa *packing*.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kidogo kabla hajanijibu. Nilipokwenda katika nchi ya Saudia Rabia mwaka huu nilipelekwa kwenye *Super Market* na yule mwenyeji aliyenipeleka pale aliniambia kitizame kiboksi hiki kina nini ndani yake.

Nilipokiangalia kimeelekea kama kimetiwa *toys* za watoto kwa vile *packing* ilivyo, lakini nilipoangalia ndani niliona ukwaju, ambao haujatolewa mabamba yake na bei yake huwezi kuamini, yaani ni kidogo sana.

Kwa hivyo, je Mhe. Waziri amejitayarisha vipi badala ya kwenda tukafuka visheti kwenye vifuko au ubuyu. Tunajitayarisha vipi na *packing* za vitu vyetu *(Kicheko/Makofi).*

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Mwenyekiti, mafunzo ya *Packing* tumekuwa tukiyatoa muda baada ya muda. Tukiangalia biashara zinazokwenda nje hivi sasa zote wahusika wote wamepitia mafunzo hayo. Kwa mfano, wanaouza viungo nje walikuwa wakiuza kwenye hizo *packing* ulizozisema za ubuyu au vitu vyengine vinavyofungwa kwenye mifuko ya *plastic*.

Lakini hivi sasa wamefanya packing nzuri za maboksi na ukiona utadhani hizo *toys* ulizoziona. Kwa upande wangu sitodhani *toys* maana yake ninatasoma kwa sababu zile *packing* zina maelezo yote ya kile kilichomo ndani.

Vile vile wanauza bidhaa za chupa na wao pia wana-packing nzuri tu na wanatumia chupa vizuri. Isipokuwa tatizo linakuja wengi wao niseme baada ya mafunzo wanashindwa na mtaji wa kununua vile vifaa vya kufanyia *packing*, kama vile chupa au ku-*print* maboksi ama ku-*print* karatasi zao maalum za kufanya hivyo.

Kwa wale walioingia *stage* ya kwanza wanatumia *computer* kwa ajili yaku-*print* lebo zao na kuweka kwenye *packing* zao. Lakini suala la mafunzo ni suala linaloendelea na tutaendelea kutoa mafunzo, bila ya shaka tutaendelea kutafuta mitaji, ili kuwawezesha waweze kufika hatua hiyo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na kutaja eneo ambalo wameomba.

Lakini kuna eneo ambalo ni zuri na tayari lina majengo, maji yapo pamoja na umeme na eneo hilo liko sehemu ya Kipandoni Mchekeni. Hivi Mhe. Waziri haoni eneo hili ni vizuri kuliimarisha zaidi, ili liweze kutumika kwa ajili ya maonesho hayo.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Mwenyekiti, eneo la Kipandoni lilitengwa kuwa ni eneo la bidhaa za kitalii na kuondosha mapapasi ambao wanasumbua kwenye maeneo ya baharini katika fukwe za Kiwengwa mpaka Pwani Mchangani.

Eneo lile wizara ilijitahidi kujenga vibanda kumi pamoja na kuweka fursa zote ambazo Mhe. Mjumbe amezitaja.

Jambo la kusikitisha ni kwamba Halmashauri ambayo tumeikabidhi pamoja na Serikali ya Wilaya hawalitumii eneo lile na badala yake wakatoa fursa kwa wananchi kuchoma, ili wasilitumie na mapapasi waendelee kubakia baharini.

Kwa hivyo, ninawaomba Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini pamoja na Serikali ya Wilaya kulifanyia kazi eneo lile na kuhamisha mapapasi katika ufukwe wa bahari kwa sababu ni kero.

Katika hili ninategemea nguvu kubwa kutoka kwake Mhe. Mwakilishi *(Kicheko/Makofi).*

**Nam. 65**

**Mafanikio ya Wizara katika Kukuza Biashara na Kutafuta Masoko**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Kny: Mhe. Anaclet Thobias Makungila) –** Aliuliza:-

Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji imefanikiwa kiasi gani katika kukuza biashara na kutafuta masoko kwa bidhaa za Zanzibar na kutoa taarifa za kibiashara kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 65 kama ifuatavyo:-

Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji imefanikiwa kukuza biashara na kutafuta masoko ya bidhaa kuanzisha na kukiendeleza Kituo cha Habari za Biashara.

Wizara ikishirikiana na *UNDP* kupitia mradi wa JP5 imekiimarisha kitengo hicho kwa kuanzisha mtandao wa taarifa za biashara (*data base)* pamoja na kutoa vipeperushi mbali mbali ambayo vinasambazwa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Zanzibar Chamber of Commerce wizara huwa inawapatia wafanyabiashara pamoja na wajasiriamali mafunzo ya uchambuzi wa miradi, maandalizi ya mpango wa biashara, utafutaji wa masoko. Mengine ni kuyatarisha bajeti na kuwawezesha kufanya mijadala au mapatano, pia kupanga bei pamoja na kutafuta mitaji au kuwasaidia kutafuta mitaji.

Napenda kuchukua fursa hii kutoa taarifa kwamba mafunzo hayo yanaendelea na hivi ninavyozungumza leo tuko Kaskazini Pemba kwa ajili ya kuendesha mafunzo haya.

**Mhe. Mohamed Ali Salim:** Mhe. Mwenyekiti ahsante. Katika masoko ya nje kuna mambo muhimu ambayo huwa yanaangaliwa kwenye bidhaa, ili iweze kununuliwa. Miongoni mwa mambo hayo moja ni kuwa na *seal*.

Hivyo, naomba kujua kutoka kwa Mhe. Waziri, wafanyabiashara wa hapa Zanzibar wanao uwezo wa kuweka *seal* kwenye biashara zao, ili inapofika kule inakouzwa watu wakaitia kwenye *computer* na kuonekana hii ndio nzima, ama si sahihi ama ndiyo yenyewe ya asili pamoja na mambo mengine.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba s*eal* ni moja miongoni mwa sifa ya bidhaa inayopelekwa nje, ili ijulikane. Vile vile wizara inalitambua tatizo la wafanyabiashara kutokuweza kuweka s*eal*, wafanyabiashara wachache sana ndio wanaoweza kufanya hivyo. Kwa sababu wanapokwenda kutafuta *TBS* wanatakiwa kulipa shilingi milioni 3 na nusu, ili kuweza kupatiwa *seal*.

Isipokuwa hivi sasa wizara hivi sasa inafanya mazungumzo na *TBS*, ili wafanyabiashara wa Zanzibar, yaani *Private Sector* ya Zanzibar iwe na utaratibu maalum wa kununua *seal* kwa pamoja na wengine watakaokwenda kuomba se*al* idadi hii ya fedha iwe imepungua, kwa sababu zitakuwa kwenye mradi moja. Kwa hivyo, hili tunalijua na tunalifanyia kazi na *TBS*

**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Wakati wa ukoloni Maruwehi wakiuza chokaa nchi za nje na maghala mengi yako kule Saateni. Je, yale masoko ya chokaa nje hivi sasa hayapo.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Mwenyekiti, masoko ya chokaa nje yapo, lakini kuna viwango maalum vinahitaji kufikiwa, ili chokaa ikubalike kuuzwa nje. Kwa habati mbaya hakuna mfanyabiashara aliyejitokeza kutaka kuuza chokaa nje.

Vile vile chokaa inatokana na kukatwa na kung'olewa kwa rasilimali tulizonazo, yaani mawe na kukata miti kwa ajili ya uchomaji. Kwa hivyo, mauzo ya chokaa nje ni kuharibu mazingira yetu hapa kisiwani. Kwa maana hiyo, hata kama atatokea mfanyabiashara nikiwa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji sidhani kama mradi huu nitauruhusu.

**Nam. 13**

**Kuinua Vipaji vya Wanamichezo Chipukizi**

**Mhe. Said Khelef Ali –** Aliuliza:-

Chimbuko la wanamichezo wazuri huanzia maskulini, kwa sababu ni sehemu inayotumiwa na wataalamu kuibua vipaji mbali mbali vya wanamichezo.

(a) Je, wizara yako imejipanga vipi kuhakikisha vipaji vya wanamichezo chipukizi vinainuliwa ipasavyo, ili taifa letu liwe na wanamichezo bora.

(b) Kwa kuzingatia kuwa walimu wengi hawana ujuzi wa michezo ya mpira wa miguu, riadha, *netball* na michezo mengine. Je, wizara yako itachukua hatua zipi kuwasaidia, ili kuwapatia utaalamu utakaowasaidia vijana wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo-** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nikubaliane na Mhe. Mjumbe kuwa wanamichezo wazuri na vipaji huanzia ngazi za skuli.

(a) (i) Moja kati ya mipango hiyo ni utekelezaji wa Sera ya Michezo, ambayo ilipitishwa rasmi na Baraza la tukufu Wawakilishi na sera hiyo inaelekeza kuwepo kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, katika kuhakikisha kuwa inakuwepo mitaala inayojumuisha michezo nakutumia wataalamu wa michezo kufundisha michezo mashuleni.

Hata na Sera ya Elimu nayo inacho kipengele maalum cha michezo katika skuli zetu na yapo mashirikiano ya karibu kati ya wizara zetu hizo mbili.

(ii) Njia ya pili ambayo wizara yangu itatumia ni kuimarisha
*Academia* za michezo za binafsi na zile za serikali kwa kwa kuwapa vibali na kuwatambulisha rasmi kiserikali pale wanapoomba misaada. *Academia* hizo zinazoanzishwa hapa Zanzibar huwa na vituo mbali mbali vya kuibua vipaji, kuinua na kuendeleza vipaji vya vijana wadogo kutoka sehemu mbali mbali za nchi.

Miongoni mwa *program* ya *Academia* hizo ni Mradi maalum unaojulikana *Olympic Africa*, ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashirikiana na Shirikisho la Kimataifa la *Olympic* ulimwenguni kuanzisha *Academia* hiyo huko Dole.

(b) Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imechukua hatua kadhaa za kuhakikisha kuwa walimu wa michezo tofauti wanapatiwa mafunzo ya kuwaendeleza wao binafsi pamoja na mafunzo yatakayowasaidia vijana wetu. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeleta nchini wakufunzi kutoka nchi zifuatazo: Wamekuja Wakufunzi kutoka Ujerumani, Misri, Japan, Afrika ya Kusini, Marekani na Shirikisho la Mchezo wa Mpira Duniani *FIFA*, ili kuendesha Mafunzo ya Uwalimu na kwa walimu na Madaktari kwa ajili ya afya ya michezo. Michezo ambayo ilihusika katika mafunzo hayo ni michezo ya Riadha, *Netball*, Kuogelea, Mieleka, Judo, Mpira wa Miguu na *Hockey* na madaktari mbali mbali wa michezo ambao walishiriki semina hizo.

Wizara yangu inaendelea na mafunzo ya kuwapatia mafunzo walimu wetu katika skuli mbali mbali kupitia wakufunzi wa ndani na nje ya nchi pale uwezo wa kifedha unapopatikana.

Hivi karibuni tunategemea kupata walimu wamichezo ya *Volleyball* na Riadha kutoka Cuba, ambao ni mabingwa wa michezo hiyo ulimwenguni na watakuja kufundisha vijana wetu pamoja na walimu wa michezo katika skuli.

Sambamba na hilo tayari hatua za kuwapatia makaazi na usafiri wa hapa nchini umeshakamilika. Vile vile kila mwaka Zanzibar hupokea *scholarship* mbili kutoka Cuba ambazo ni za walimu wa michezo ambao wanakwenda kusomea *degree* za kuja kufundishia michezo hapa Zanzibar. Ahsante sana.

**Mhe. Mohamedd Ali Salim:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Ni mwaka gani wa mwisho waliokuja walimu na wamichezo gani, walifundisha kwa muda gani?

(b) Mafunzo yanapotolewa kwa walimu wa michezo katika skuli zetu. Je, ni skuli zote wanapata nafasi hiyo au kuna skuli maalum zinazobahatika. Kama kuna skuli maalum zinazobahatika je nafasi hizo hugawanywa kwa skuli za mijini na vijijini au huchukuliwa walimu wa skuli za mjini.

(c) Je, baada ya mafunzo haya ufuatiliaji unaonesha vipi. Kuna maendeleo ya yale yaliyosomwa na yaliyofundishwa au yale yaliyosomwa yamewekwa vikapuni hayatumiki.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti,

(a) Kwanza kabisa sitosema kuanzia mwaka gani au mwisho ilikuwa ni mwaka gani. Kwa sababu hivi sasa tunaowalimu wafuatao ambao wapo hapa Zanzibar wanatumika kwa ajili ya Wizara yetu ya Habari, Utamaduni na Michezo katika michezo ya kawaida, sambamba na hilo, wamepangiwa *program* nyengine ya kwenda kuwafundisha walimu katika skuli mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuitaja michezo yewenye pamoja na hao walimu waliokuwepo. Tunae mwalimu wa Mchezo wa *Basketball* ambaye yupo hapa Zanzibar na yeye amekuja kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na sio Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, alipitia Afisi ya Katibu Mkuu.

Kwa hivyo, sisi kama Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo tunamtumia katika Mchezo wa *Basketball* kwa timu zetu za taifa za *Basketball*, lakini anatokea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hata kibali chake cha ukaazi, yaani *work permit* kwa hapa Zanzibar barua imetolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya mchezo huo na anatumika muda mwingi zaidi na wizara ya elimu. Isipokuwa sisi humtumia kwa timu zetu za taifa kwani hivi sasa zinajitayarisha kwa ajili ya kushiriki mashindano ya taifa.

Pili ni Daktari kutoka nchini Misri ambaye ameletwa na Ubalozi Mdogo wa Misri nchi Zanzibar na huyu daktari yupo na tayari ameshatoa semina kadhaa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kuwafuata wale wachuaji wa mambo ya michezo. Afisi yake hivi sasa tumempatia katika Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Kariakoo na anaendelea na *program* yake maaalum ya kutoa mafunzo hayo.

Tatu, tunae mtaalamu bingwa duniani wa Judo ambaye anatoka Japan ninadhani mnamuona kwenye vyombo vya habari anaitwa Shima Uko na anatoa mafunzo tofauti kwa Timu ya Taifa ya Judo Zanzibar na pia anatoa mafunzo ya kuwachukua watoto wapya. Vile vile anatarajia kupanga *program* maalum ya kuzunguka kwenye skuli mbali mbali kujaribu kushajihisha mchezo huo uwe unachezwa.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni mifano ya michezo, lakini iko mingi. Pia tunae Kocha wetu kutoka Misri ambaye anaitwa Badru Al-din yeye

amekuja kwa ajili ya Timu ya Taifa ya Zanzibar, lakini muda ambao timu ya taifa haipo kambini na haina matayarisho yoyote, tumemuamuru kuanzisha program za kwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kuwafundisha walimu wa michezo wake kama yeye, yaani makocha wetu wa baadaye kwa mpira wa miguu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, skuli zote zinapewa kipaumbele cha kupata mafunzo haya. Lakini tunachokifanya hivi sasa kutokana na uwezo uliokuwepo, yaani walimu hawa hawendi skuli moja moja, isipokuwa kinachofanyika kila skuli huombwa kuleta mwalimu wa mchezo wa mchezo au michezo wa skuli ile ambaye anashiriki kwenye semina pamoja na mafunzo hayo.

Semina hizo huwa kila mara hufanyika katika Uwanja wetu wa Amani kwa hapa Zanzibar. Hivi karibuni mwezi uliopita Disemba ilifanyika semina kubwa pale Uwanja wa Gombani Pemba ambayo iliwashirikisha walimu kutoka skuli mbali mbali.

(c) Kuhusu takwimu zinaonesha vipi. Kwa kweli zinaonesha kwamba kuna mapungufu makubwa sana kwa upande wa skuli. Kwa sababu wale walimu wakeshapatiwa yale mafunzo na wakeshatoka kwa ajili ya kurejea skuli, basi mara nyingi skuli zile zinakuwa hazina vifaa vile vya michezo.

Kwa mfano, hivi karibuni tumepata malalamiko kutoka skuli tatu ambazo wamefundishwa vizuri sana Mchezo wa *Volleyball*, lakini skuli zile hazina hata zile vyavu za kuchezea mchezo huo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi ninakuomba kwa pale Mkoani na wewe kama utaingiza jitihada zako angalau kwa kuwapatia vyavu pamoja na mipira ile *Volleyball*, basi utatusaidia sana ili hawa walimu waweze kupata kufundisha kwa vitendo badala ya kinadharia tu.

Kwa upande wetu tutajitahidi kuendelea kutafuta misaada mbali mbali ambayo itaweza kupatikana. Isipokuwa suala la msingi ni kushirikiana, ili na wewe uchangie katika suala la michezo kwa ajili ya kuendeleza michezo hiyo na zile takwimu tunazotolea mafunzo ziweze kufikiwa.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, walimu wote alioeleza Mhe. Waziri sina matatizo nao na mimi katika shughuli ambazo nimeshiriki katika mwaka huu kwenye mashindano ya Afrika ya Mashariki na Kati huko Uganda, basi huyu kocha Mmisri nilikua nae, ni kocha mzuri na mzalendo kweli kweli kwa nchi yetu ya Zanzibar.

Naamini na Zanzibar ina vipaji vizuri sana katika mpira wa miguu, vijana wetu ambao wameshiriki katika mashindano hayo walikuwa ni wachanga kabisa ukitoa wachezaji watatu tu, wa kwanza *captain* Abdi Kassim *(Babi), wa* pili Nabil Haroub (Canavaro*)* na wa tatu ni mchezaji wa Chuo cha Mafunzo, jina lake kidogo limenitoka ambae kwa sasa hivi kapewa *captain* yeye ni Agree Morris, kijana mzuri sana, hata mwenyewe Marcio Maximo kamuona na kipa wetu akasema hawa wachezaji watanifaa katika kuongezea timu ya Taifa ya Zanzibar.

Suala langu lipo hapa baada ya kutoa maelezo marefu ili wananchi wapitie na waelewe kitu gani kinaendelea. Kuna tatizo ambalo limejitokeza naiomba Wizara kama ifuatavyo kama atanipa majibu Mhe. Waziri, kikwazo cha kutoonekana wachezaji wetu kushiriki katika timu ya taifa ni ukosefu wa timu tatu bora za Muungano kati ya Bara na Visiwani, ile ligi ya muungano inaleta matatizo ya kutokuonekana vipaji vya wachezaji wetu wa Zanzibar.

Je, Wizara ina mpango gani wa kurudisha mashindano yale ili vipaji vile vionekane Bara, na hapa visiwani akija kocha mkuu wa Taifa awaone vijana wale ili wapate soko katika timu ya taifa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Kabla sijamjibu Mhe. Ali Suleiman Ali naomba nimpongeze sana kwa suali zuri sana ambalo ameliuliza, ni suala muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti jana asubuhi kwa bahati nzuri nilibahatika kuwa na kikao kifupi cha nusu saa na kocha wa Tanzani Marcio Maximo, katika suala kubwa tuligusia ni hili na naomba niseme wazi katika Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti kwamba Marcio Maximo alikuwa analalamika sana, kwamba *TFF* haitusaidii sisi huku Zanzibar, nadhani na hilo wajumbe mtakubali kwa sababu zile gharama zake za kwenda kuibua vipaji Tanzania nzima zinatolewa na *TFF*. Marcio Maximo anapewa posho lake la kuzunguruka Tanzania nzima kwenda kuibua vipaji, yaani anakwenda Arusha, Mwanza, Shinyanga na kwengine kote katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, isipokuwa hapa Zanzibar hafiki.

Sasa kitu alichoniomba amesema nakuomba Mheshimiwa nyinyi mjaribu ili vipaji vyenu viweze kuonekana tufike mpaka Pemba nina hamu kwa sababu nakusikia na sijawahi kufika hata mara moja na mimi nimepewa jukumu la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu ile timu ni ya Taifa. Kwa hivyo, ametuomba sisi sasa tujitahidi kutafuta bajeti zetu wanyewe tumlete, ili tuweze kuzunguruka nae kote kwa sababu wenzetu hawatusaidii. Hilo nasema wazi katika Baraza lako tukufu. Tumeshaomba mara kadhaa, lakini hawataki kutusaidia wanasema zile ni bajeti zao na kuna pesa ambazo wanapata kutoka FIFA ambazo zinatakiwa zitumike kote bado hizo hatuzipati moja kwa moja.

Sasa mimi nachukua ahadi kwamba huyu Marcio Maximo tutamleta hapa Zanzibar kwa pesa zetu wenyewe, tutazunguruka nae, na tutamleta kwenda kuangalia ligi mbali mbali pamoja na hizo zitakazochezwa Pemba na mechi nyingi safari hii zitachezwa Pemba kutokana na uwanja wa Amaan kufanyiwa ukarabati au matengenezo. Kwa hivyo, huyu bwana tutamleta na kama tulivyowahi kumleta safari moja nadhani mlimuona hata kwenye TV, alikuja hapa akazungumza na watu mbali mbali na masuala hayo ni miongoni mwa wanamichezo wengi yanawaudhi kwamba hawatoki wachezaji, wanaotoka ni wale ninaowaona kutoka timu za Simba na Yanga akasema kwa sababu hana njia nyengine ya kuwaona hao wachezaji.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru mwaka huu Mjomba Mhe. Ali Suleiman Ali *(Shihata)* umeeleza kwa uwazi kwamba hilo suali limeonekana na nachukua ahadi hiyo tutamleta kocha huyo kwa ari yetu sisi wenyewe na tutazunguruka nae na kuibua vipaji hapa Zanzibar. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa hii kauli aliyotoa Mhe. Naibu Waziri ni kauli nzito sasa hili ni kero, sasa wahusika Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Hamza Hassan Juma kazi kwenu, ikiwa Mheshimiwa katoa kauli hebu lifuatilieni.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kabla ya kuuliza swali langu la nyongeza lenye vifungu a na b napenda kutoa shukurani kwa maelezo ya Mhe. Waziri kama alivyoeleza na labda sasa atakubaliana na kauli zetu kwamba ile timu iliyokuweko kule sio timu ya Taifa ya Tanzania, lakini ni timu ya taifa ya Tanganyika, na uthibitisho ni kwamba *TFF* hata kutusaidia huku Zanzibar hawatuingizi, tumefurahi kupata hiyo kauli ya Waziri pamoja na maelezo ya Kocha Marcio Maximo atakuwa anaipinga tena kauli yake ya kuwa Zanzibar hakuna vipaji sasa amekubali kwamba huku hakuna siasa kuna mchezo na vipaji vipo.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu la nyongeza kuhusiana na masuala haya ya kimichezo pia nimpongeze kwa juhudi zake Mhe. Naibu Waziri, na swali langu litalenga katika juhudi ya kuwa na wakufunzi wengi ambao watatufanyia kazi nzuri sasa swali langu lipo hapa.

a) Pamoja na kuwa na wakufunzi pamoja na madaktari Je, kupitia Wizara yake wamejiandaa vipi kuhusiana na viwanja kwa ajili ya hiyo michezo, maana yake walimu tayari wapo na vijana wa kufanya hizo shughuli wapo tunakwenda je katika mpangilio mzima wa viwanja ni juhudi gani zimechukuliwa na labda tumefika wapi.

b) Pamoja na mafunzo hayo ya kimichezo suala zima la waamuzi, michezo ni mingi na bila ya shaka kila mchezo una waamuzi wake na sheria zao, je tunasubiri waamuzi kutoka Tanganyika au kutoka nje ya nchi au tuna mpango gani wa kuwa na waamuzi wetu katika program nzima ya kuleta wataalam kutoka nje.

c) Mwisho kwa sababu mtu unapokuwa barabarani basi chochote kinaweza kutokezea, tumeambiwa kuna madaktari wapo je suala zima la vifaa vya matibabu na madawa limeangaliwa vipi na labda liko katika hali gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti kabla sijamjibu naomba tena niweke sawa zile *comment* alizotoa kabla ya kuuliza swali lake.

Alichosema Marcio Maximo ni kwamba wachezaji wa Zanzibar njia pekee ninayoweza kuwaona mimi ni kupitia timu zinazocheza Bara yaani Simba na Yanga, kwa hivyo ile bado ni timu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mimi sitaki kuisusia ni timu yetu ya Taifa, lakini kuna wachezaji hawa wawili Abdi Kassm na Nabil Haroub ambao kawaona kutokea huko huko.

Lakini anachosema vipo vipaji vingi safari hii ndio mara ya kwanza kaviona kutoka Timu ya Taifa ya Zanzibar, lakini hana njia ya kuviona zaidi akiwa yuko huko mpaka aje huku kwa sababu wale hawachezi katika zile timu mbili za Simba na Yanga mpaka aje huku ndipo atakapoweza kuwaona.

Kwa hivyo, bado ile ni timu ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini tunachotakiwa sisi ni kupigania haki zetu ili tuweze kuwemo ndani kikamilifu, tukiisusia tukasema hiyo ni timu ya Tanzania Bara au timu ya Tanganyika ile ni timu ya Tanzania tunachotakiwa ni kupigania haki zetu ili tuwemo ndani. Kupigania haki zetu za pesa za *FIFA* na ndani ya *TFF* angalau kuwa na wajumbe wawili wa bodi kutoka Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti hili nalipitisha katika hizo kero zinazozungumzwa, tuwe na wajumbe wawili angalau ile misaada iletwe na Zanzibar.

Kwa sababu katika ratiba ya *TFF* hakuna nafasi ya mjumbe wa bodi kutoka Zanzibar, lakini katika sheria ya Baraza la Michezo la Tanzania kuna sheria

inasema kuna mjumbe atatokea Zanzibar na mjumbe huyo yupo, lakini katika shirikisho la mpira wa miguu hamna sheria hiyo.

Pili Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba vipaji vipo Zanzibar na hilo limeshaonekana kuhusiana na wakufunzi, vifaa na madaktari hili Mhe. Mwenyekiti tutaendelea kufanya *program* maalum ili kuwashajihisha hao madaktari, isipokuwa kuna mapungufu ya vifaa kama nilivyosema hapo awali kwamba tunakuombeni na nyie waheshimiwa Wawakilishi katika majimbo yetu, katika skuli zenu na vijana wenu mjaribu kusaidia vifaa vya michezo. Mhe. Omar Ali Jadi yuko *active,* Mhe. Ali Omar Shehe kachezesha ligi hivi karibuni, Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mwinyi Haji katika jimbo lake na wengi wengineo ambao wanaendeleza michezo katika majimbo yao.

Mhe. Mwenyekiti, suali jengine nililoulizwa ni kuhusu viwanja.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti niliulizia vifaa vya matibabu kwa sababu vifaa vya michezo tunajitahidi kupeleka mipira, jezi na vitu kama hivyo lakini katika kucheza wakati mwengine wanaumia vibaya. Sasa nilikuwa naulizia vifaa vya matibabu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Nilikuwa nakuja huko huko sijafika tu Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na vifaa vya matibabu hilo liko moja kwa moja chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na naamini pale ambapo sisi tunaomba kutoka kwao kwa ajili ya ile *medical kit* kuna *first Aid Kit* mbali ambayo anakuwa nayo daktari wa michezo pale kwenye uwanja, wengine wanakuwa na mabegi makubwa zaidi *medical kit*.

Mara nyingi timu kisheria inatakiwa kuwa na daktari wa dawa za michezo saa zile mara nyingi zinakuwa zinapatikana, lakini baada ya hapo inapotokezea mchezaji kuumia mfano mguu kuvunjika na kadhalika lile linakuwa moja kwa moja la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tunampeleka hospitali na Mhe. Waziri ameeleza kwamba akihitaji kupelekwa nje wanampeleka kama alivyoeleza leo asubuhi wakati akijibu mswali yake.

Kuhusiana na suala la waamuzi naomba tena na tena nikuombeni Wawakilishi pamoja na wananchi wa Zanzibar naomba mjiotokeze kwa wingi kwenye mitihani ya waamuzi, mitihani ya *FIFA* inapokuja kufanywa hapa Zanzibar hakuna watu wanaojitokeza kuwa waamuzi, waamuzi wetu wote sasa hivi ni wa umri mkubwa.

Mhe. Hafidh Ali Tahir ambe hachezeshi, lakini ni muamuzi wa ngazi za *FIFA*, ndugu Juma Ali David ni mwamuzi wa *FIFA* ambae hivi karibuni alipata matatizo ya kuumwa, lakini nasema hatuna waamuzi wanaojitokeza kwa wingi.

Kwa hivyo, hilo sio kosa letu sisi kama Wizara sisi tunajaribu kushajihisha kupitia wawakilishi tunaomba wananchi wenu muwaambie wajitokeze kwa wingi kuja kufanya mitihani ya waamuzi, mitihani hii hufanyika mara mbili kwa kila mwaka.

Kuhusiana na viwanja vya michezo hivi sasa Wizara haina mamlaka moja kwa moja katika viwanja vya michezo, viwanja vingi vya michezo vipo moja kwa moja chini ya Wizara ya Elimu kwa zile skuli zao zenye viwanja vya michezo, au kwenye Tawala za Mikoa yaani kwenye maeneo mfano katika jimbo langu kuna kiwanja cha Michezo cha Bintiamrani, Kuna kiwanja cha Taifa ya Jang'ombe wapo wenyewe hapa na viwanja vyengine mbali mbali na Wandaras na pale Migombani.

Kwa kuwa lilitolewa hili agizo na Mhe. Waziri, kwamba kila mwenye kiwanja kama ni timu au klabu kwenye eneo lile au serikali za mitaa waje wakiandikishe na kukisajili ili kisijekuvamiwa kwa mambo ya majenzi, lakini viwanja viko moja kwa moja kwenye mamlaka yenu hata nyinyi Wawakilishi kupitia ngazi za majimbo. Ahsante sana.

**Nam. 33**

**Serikali Kushindwa Kupeleka Waandishi wa Habari Katika Mikutano Muhimu**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu –** Aliuliza:-

Kwa kuwa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yapo Arusha Tanzania; Na kwa kuwa mara kwa mara Vikao na Mikutano ya Jumuiya hiyo pamoja na mikutano mingine muhimu ya Kimataifa kama vile Mkutano wa *LEON SULLIVAN* hufanyika hapo; Na kwa kuwa nchi nyingi zikiwemo za ndani ya Jumuiya hiyo na za nje ya Jumuiya hupeleka waandishi na wapiga picha wao katika mikutano hiyo na vikao hivyo isipokuwa Zanzibar ambayo nayo ikiwa sehemu ya Mwanachama wa Jumuiya hiyo.

(a) Je Mhe. Waziri ni sababu gani inayoifanya Serikali kushindwa kuwapeleka waandishi wake kwenye mikutano hiyo kila inapofanyika:-
   - (i) Ukosefu wa fedha.
   - (ii) Kutokuwaamini waandishi wake.

(iii) Ni kuto kujua na kuuona umuhimu wa mikutano hiyo au

(iv) Ni kwa sababu Zanzibar ina wakilishwa na Tanzania kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano.

(b) Mhe. Waziri huoni kama hali hiyo inawafanya waandishi wetu wawe wanavunjika moyo, wajione dhalili, wanyonge na wajihisi kuwa wanapuuzwa na kudharauliwa.

(c) Je Mhe. Waziri huoni kwamba jambo hilo linawafanya waandishi wa vyombo vyetu vya Habari waonekane wanatumikia vyombo vya daraja la pili au la tatu mbele ya vyombo vya Habari vyengine, na huoni kwamba tunavijengea mazingira mabaya mbele ya jamii yanayofanya vionekane kuwa ni vyombo vya kuripoti *MAWIO* na *MATUKIO* yanayojitokeza ndani ya Zanzibar peke yake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa nataka nipongeze Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu kwa kuvunja rekodi ya kuuliza swali refu kwa Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo tokea mwaka 2005, kwa hivyo hili limevunja rekodi kwa urefu.

Mhe. Mwenyekiti,

(a) Ukosefu wa fedha ni sababu kubwa inayozuia waandishi wa Habari wa Zanzibar kushiriki katika mikutano hiyo, kwani kama tunavyoelewa Bajeti za Taasisi za Habari za Serikali ni finyu mno ikilinganisha na mahitajio yake ikiwemo safari za Nje na sehemu nyengine za Tanzania kikazi, hivyo vyombo hivi uwezo wake ni mdogo na ni mara chache hasa inapotokezea shughuli maalum ya Kitaifa ndiyo huweza kufikia na kutekeleza majukumu yao. Fedha hizo huombwa katika bajeti kuu, lakini kutokana na uzito wa mwanzo ama kipaumbele juu ya sekta nyengine muhimu kama vile Afya, Maji, Kilimo n.k huwa tunapata kasoro katika kasma hii.

Napenda kulihakikishia Baraza hili kuwa Waandishi wetu wa Habari wengi wao ni makini na waliobobea katika fani hiyo, hivyo wanaaminika na wanao uwezo mkubwa wa kufanyakazi hiyo katika Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na vyenginevyo vyote vya Kimataifa na Kitaifa. Mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia waandishi wetu wa habari kutoka hapa Zanzibar wakitumikia mashirika mengine

mbali mbali duniani ya kitaifa Tanzania na kimataifa wakiwa kama waandishi wa habari kwa muda, au kwa mkataba maalum kutokana na umahiri wao huo. Baadhi ya nchi ambazo zina waandishi wetu wa habari ni Ujerumani, Uingireza, China, Marekani na Tanzania Bara. Umuhimu wa mikutano hiyo unaeleweka na viongozi wa vyombo vyetu vya habari wanalielewa kama vile ilivyo tatizo la kuripoti habari katika vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Dodoma.

(b) Suala la habari si la Muungano, lakini pia hiyo haizuii vyombo vya Habari vya Zanzibar kuchukua habari katika mikutano hiyo ya Jumuiya na Taasisi nyengine zozote za ndani na nje ya Nchi. Kama wanavyofanya wao kwa habari za hapa Zanzibar mashirika mbali mbali yanakuja kuchukua habari hapa Zanzibar, mfano mzuri ni katika sherehe za Mapinduzi zilizofanyika hivi karibuni huko Pemba ambapo TBC ambayo zamani ilikuwa TVT wakishirikiana na TVZ kuchukua sherehe hizo kupitia TVZ moja kwa moja na kuonyeshwa sio Tanzania tu lakini dunia nzima kupitia satalaiti ya TVT.

Kwa vile suala la uhaba wa fedha linaeleweka vyema kwa viongozi wa taasisi hizi, hali hiyo haikufanywa siri na Waandishi wetu wa habari wameelezwa na wanaifahamu, na kuelewa kuwa uwezo utakaporuhusu watashiriki katika vikao hivyo, sioni kama wanalichukulia kama alivyouliza Mheshimiwa aliyeuliza suala hili.

(c) Waandishi wetu wa habari hawaonekani kama wanatumikia vyombo vya habari vya madaraja ya pili au tatu , vyombo vya habari havijaekewa madaraja kama timu za mpira zinavyowekewa na ZFA. Vyombo vyetu vya habari viko mahiri na vinatoa habari za Zanzibar mwanzo na habari hizo hutumiwa na vyombo vyengine vya sekta binafsi, hivyo huwa ndio ”*source*” kubwa inayoaminika na vyombo vyengine mbali mbali hapa nchini na nje ya nchi pamoja na ile ya Gazeti letu la Zanzibar Leo, liko mbele sana kwa kutoa habari za Kimataifa na habari za michezo ya Ligi za zote za hapa nchini na zile za nje pamoja na ile ya Uingereza ambayo inaashiria kwamba Livepool itakuwa bingwa. Licha ya kutoa habari za ndani za maendeleo na uchambuzi.

Aidha, kwa sasa ninaomba niwashauri viongozi wa Taasisi nyengine ambao watakuwa wanahusika na vikao vinavyoendelea vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, washirikiane na Wizara yangu ili kuangalia uwezekano wa wanahabari wetu kuongozana nao kila wanapohusika na mikutano hiyo kwa lengo la kuwapatia taarifa Wananchi wa Zanzibar,ambao wanavitegemea zaidi vyombo hivyo vya hapa Zanzibar.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:
Nafikiri atakubaliana na mimi kwamba vyombo vya habari vimepoteza mvuto kwa wasikilizaji na watazamaji na badala yake sasa watu wengi wanapendelea zaidi vyombo vya Jamhuri ya Muungano na vyombo vya kimataifa.

Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuwaweka wananchi katika mazingira kama haya wasikilize habari zaidi za nje kuliko ambazo zinawahusu ambazo sio nzuri katika maendeleo ya taifa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kwamba nitapingana na Mhe. Haji Faki Shaali kutokana na *survey* ambayo imefanyika hapa Zanzibar na *survey* hiyo ni kubwa na vile vitabu tumevitoa, najua Mhe. Haji Faki Shaali vitabu vyote anavipitia kuanzia *heading* mpaka ukurasa wa mwisho wa mchapishaji.

Sasa naamini na hicho hakijakupita. Katika *survey* kubwa iliyofanyika ya aina yake kwa hapa Zanzibar vyombo vya habari vya Zanzibar ndivyo vilivyokuwa vinaongoza kusikilizwa na Wazanzibar nayo ni STZ, TVZ na Gazeti la Zanzibar Leo. Nikataja Nipashe ilikuwa namba tatu katika *survey* hiyo iliyofanyika na ushahidi upo ni hicho kitabu na hiyo *survey* ilidhaminiwa na Shirika la *UNDP* na ilichukua wataalam sio wa kujipigia debe kama ninavyopiga debe mimi kwa vyombo vyangu ambavyo vipo katika Wizara yangu.

Hiyo ilikuwa ni *indipendent survey* ilifanyika na Mhe. Haji Faki Shaali kama anataka kopi zaidi ya vitabu hivyo bahati nzuri tunazo na tunaweza kuziwasilisha. Kwa hivyo, naomba nikatae kwamba hilo halipo na vyombo vya habari vya Zanzibar vina mvuto mkubwa na ndio vinavyosikilizwa zaidi, na mazingira aliyoyataja hayapo katika fani hiyo ya waandishi wa habari au wana habari wenyewe pamoja na wananchi ambao wanapenda kusikiliza vyombo vya Zanzibar.

**Nam. 51**
**Sanaa Zinazoharibu Utamaduni**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny Mhe. Anaclet Thobias Makungila)–** Aliuliza:-

Miongoni mwa majukumu ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ni kuzihakiki na kuzipitia sanaa mbali mbali kwa lengo la kuzifanya ziendane na maadili ya Kizanzibari na hasa ukitilia maanani wimbi la mageuzi ya kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni katika dunia hii ya utandawazi na kutoa

vibali vya maonesho ya sanaa hizo. Kuna wimbi kubwa la sanaa zinazokiuka maadili ya Mzanzibari (hasa muziki) zinazooneshwa na kusikilizwa zinazotoka hapa nchini na nchi za nje.

Vibali vya kuoneshwa na kusikilizwa vinatolewa na nani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 51 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli miongoni mwa majukumu ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonyesho ni kuzihakiki na kuzipitia sanaa mbali mbali kwa lengo la kuzifanya ziendane na maadili ya Wazanzibari kabla ya kuoneshwa au kusikilizwa na Jamii.

**Mhe. Mwenyekiti,**

(a) Kama inavyofahamika kwamba kazi za Bodi ya Sensa ni kuhakiki na kutoa miongozo hiyo pia hatua za kukataa au kuikubali sanaa husika kuoneshwa na kutooneshwa kwa kutoa fomu maalum ambazo hujazwa na kuzingatiwa maombi hayo na baadae kurudishiwa majibu.

(b) Suala la utoaji wa vibali vya maonesho yote ya sanaa hufanywa na Baraza la Sanaa, sio bodi ya sensa baada ya Baraza hilo kutakiwa lihakikishe kuwa sanaa husika imekaguliwa na bodi ya Sensa ni kweli hivi karibuni kumekuwepo na wimbi kubwa la sanaa zinazo kiuka maadili ya Mzanzibari kupitia sanaa ya muziki na nyenginezo.

Hatua hii inasababishwa na wasanii wenyewe pamoja na vyombo vya Habari kwa kutofuata taratibu zilizopo.

Hata hivyo Wizara kupitia chombo chake (Bodi) imeandaa utaratibu wa kuendelea kukutana na wenye vyombo vya Habari hapa Zanzibar kwa lengo la kubadilishana mawazo juu ya kuondoa kasoro hiyo pamoja na kutoa taaluma kwa wasanii juu ya umuhimu wa kuhakikiwa sanaa zao.

**SHUGHULI ZA SERIKALI**
**Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar.**

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mswada wetu wa kuanzisha Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar, lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa hai na uzima kwa kuhudhuria kikao hiki cha kupitisha shughuli zetu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa kumi na nne wamepata fursa ya kuchangia mswada huu nao ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu Mwenyekiti wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambae pia ni Mwakilishi wa jimbo la Muyuni.

2. Mhe. Said Ali Mbarouk Waziri Kivuli wa Mawasiliano na Uchukuzi lakini pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Gando.

3. Mhe. Abubakar Khamis Bakary\
4. Mhe. Ali Abdalla Ali
5. Mhe. Abass Juma Muhunzi
6. Mhe. Salmin Awadh Salmin
7. Mhe. Ame Ussi Juma
8. Mhe. Ame Mati Wadi
9. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
10. Mhe. Ali Suleiman Ali
11. Mhe. Ali Denge Makame
12. Mhe. Ali Mzee Ali
13. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora
14. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba niwashukuru wote waliochangia mswada huu, pia nieleze kwa ufupi kwamba lengo la mswada huu wa Sheria ilikuwa ni kuimarisha maslahi ya Zanzibar katika shughuli za usafiri wa baharini. Najua kwamba waheshimiwa wote wa pande zote mbili kwa kipindi kirefu walikuwa na mawazo ya kuwa na chombo kama hiki, hii ilitokana na mswada wa sheria au sheria yetu ya *maritime* ya mwaka 2006, lakini pia naomba nielezee kwamba sisi kama Wazanzibar tusiogope kuanzisha jambo ambalo tunahisi lina maslahi ya nchi yetu.

Kwa hivyo wakati wowote tunapoanzisha jambo inawezekana likawa na ugumu fulani lakini baadaye mambo yanaweza kukaa sawa. Baada ya maelezo hayo ya ufupi naanza kumjibu Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu Mwenyekiti wa Kamati na Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni

Mhe. Nyonje kwa ujumla alisisitiza kusimamiwa ipasavyo kwa Mamlaka itakayoanzishwa juu ya mambo yafuatayo:

1. Upotevu wa mizigo,
2. Msongomano wa abiria vyomboni na bandarini,
3. Udhibiti wa vyombo vidogo vidogo,
4. Mazingira ya bahari yadhibitiwe,
5. Elimu itolewe kwa watendaji,
6. Suala la mabaharia lisimamiwe ili kuongeza ajira na kuleta mapato nchini,
7. Pia alitaka hatua madhubuti zichukuliwe na kanuni za uokozi ziandaliwe, meli zichunguzwe zaidi ili kuzuia ajali za moto.

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mhe. Ramadhan Nyonye Pandu mwekiti wa Kamati ya Mawsiliano na Ujenzi kwa ushauri wake juu ya mambo mbali mbali yaliyoelezwa katika mswada huu. Mengi ya mambo aliyoyaeleza ni yale ambayo ameshatushauri wakati tulipokaa na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tulipokuwa tukiupitia na kuujadili Mswada huu.

Kwa vile lengo la kuanzisha Mamlaka hii ni kudhibiti shughuli za usafiri wa baharini kwa ufanisi mkubwa, hivvo ushauri wa Mhe. Mwenyekiti tunauchukua na tutaufanyia kazi katika kudhibiti upotevu wa mizigo, kupunguza msongomano wa abiria bandarini, kuweka udhibiti mzuri wa vyombo vidogo vidogo, kuimarisha mazingira ya bahari, kutoa elimu kwa watendaji na wafanyakazi, kusimamia maslahi na haki za mabaharia ili kuongeza kipato chao na kutoa fursa kwa wenye vyombo kufanyakazi kwa uadilifu haki na usawa. Aidha Mamlaka itachukua hatua madhubuti za kuweka taratibu nzuri za uokozi, kuzifanyia meli ukaguzi ili kuzuia ajali zikiwemo za moto.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri kivuli M/U na Mwakilishi wa Jimbo la Gando), yeye alikuwa na hoja nyingi kwanza aliuliza wizara imejiandaa vipi kuanzisha Mamlaka hii?

Wizara imechukua hatua za kuaandaa mazingira mazuri ya kutambuliwa Mamlaka hii duniani kwa kuwasilisha ombi IMO, kuanzisha Mamlaka ya kusimamia usafiri wa baharini. Hatua hiyo imekamilika kwa kukubaliwa na IMO pamoja na kujuilishwa nchi wanachama wa IMO kuhusu kuanzishwa

Mamlaka hii ambayo itatekeleza majukumu mbali mbali katika mikataba ya kimataifa. Aidha Wizara imewapelekeka masomoni wataalamu kadhaa katika Chuo cha *World Maritime University* cha Swiden. Vile vile Wizara imejitayarisha kwa kuitengea Mamlaka hiyo fedha, jengo na vifaa vya kufanyia kazi.

Jee, Sheria hii itaweza kufanyakazi bila ya kupingwa na sheria nyengine za Tanzania Bara kama Sheria ya *Territorial Sea ya 1989?*

Jibu ni kwamba kama nilivyosema kuwa Mamlaka hii imepata baraka za SMT kwa hivyo kwa sasa hakuna sheria ya Tanzania Bara itakayoizuia sheria hii kufanyakazi, kwani SMT ndio waliopeleka majukumu ambayo Mamlaka inatarajiwa kuyatekeleza.

Kuna wataalamu wangapi walikwenda nchi kama Panama, Liberia au Bahama kuhusu kuanzisha Open registry.

Jibu ni kwamba hakuna wataalamu waliopelekwa katika nchi hizo, hata hivyo wataalamau wawili waliwahi kwenda *Cyprus* kujifunza usajili wa meli kwa kutumia mfumo wa *Open Registry*. Aidha Wizara imeshazungumza na Malta kuhusu kumpeleka mtaalamu kujifunza uzoefu wa nchi hiyo kuhusu *Open Registry*.

Swali lake jengine, jee Mamlaka hii itafanyakazi za ukaguzi wa meli kwa kutumia *Flag State* chini ya bendera ya Zanzibar au ukaguzi wa *Port State?*

Jibu ni kwamba ukaguzi wa meli utafanywa kwa kutumia *Flag State* na *Port State*. *Flag State* kwa kutumia bandera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa meli zilizosajiliwa nchini na *Port State* kwa meli za kigeni zitakazoingia katika bandari zetu.

Mhe. Saidi Ali Mbarouk pia alitaka kujua jina hasa la Mamlaka ni Zanzibar *Maritime Authority* au *Zanzibar Maritime Regulatory Authority*.

Jina la Mamlaka ni Zanzibar *Maritime Authority* ambayo itakuwa ni Mamlaka ya kusimamia masuala ya usalama, biashara na udhibiti kwa pamoja.

Alitaka kujua Zanzibar *Maritime Zone* ni ipi?

Katika sheria hii Maneno *Zanzibar Maritime Zone* yamefutwa kwani katika Sheria Na. 5 ya mwaka 2006 kumetajwa "*Within Zanzibar*" ikimaanisha eneo la Zanzibar ambalo kwa sheria hiyo, Zanzibar imetafsiriwa kuwa ni eneo lote la Zanzibar lililotajwa katika katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Alitaka kujua kuwa vipi Mamlaka itatoa urai kwa meli wakati SMZ haiwezi hata kutoa uraia kwa wananchi wake.

Sheria ya *Maritime Transport Act 2006* imepewa mamlaka ya kutoa uraia kwa meli chini ya Usajili wa Meli wa *Tanzania Zanzibar Registrar of Shipping* na *Tanzania Zanzibar International Registrar of Shipping.* Meli inaposajiliwa maana yake ni kupewa uraia kwa kupeperusha bendera ya nchi ilikosajiliwa. Kwa hivyo Mamlaka itatoa uraia wa Tanzania kwa meli zitakazosajiliwa Zanzibar.

Alitaka kujua viwango vya mafao ya wafanyakazi melini vya kitaifa na kimataifa ni vipi?

Mhe. Mwenyekiti, viwango vya kitaifa ni vile ambavyo vitapangwa na Mamlaka na vya kimataifa ni vile vilivyowekwa na *International Labour Organization (ILO) au International Transport Federation (ITF)*

Pia Mhe. Said Ali Mbarouk alitaka kujua jee Zanzibar imepewa Mamlaka ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa?

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, Serikali ya Muungano ndio yenye Mamlaka ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa. Hata hivyo Zanzibar inaipitia mikataba kwa pamoja na SMT na kutoa mapekendekezo yake ndio baadaye inaridhiwa na Tanzania kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia alitaka kujua mbona Mwenyekiti wa Bodi hakupangiwa vigezo vya kuchaguliwa?

Mhe. Mwenyekiti, Rais amepewa uwezo wa kumchagua mtu anaemtaka kwa kutumia katiba ya nchi na busara zake. Utaratibu huo utakapokubaliwa na Serikali tutafanya hivyo

Lakini pia Mhe. Said Ali Mbarouk alitaka kujua kuhusu Mkurugenzi Mkuu kuteuliwa na Rais alisema kwamba utaratibu hii ni wa kizamani, hivyo Bodi itoe nafasi hiyo itangazwe ili watu wote waweze kuomba.

Lakini bado serikali haijaweka utaratibu wa viongozi wakuu wa taasisi za serikali kama Mkurugenzi Mkuu kuchaguliwa kwa nafasi za kutangazwa na kuchaguliwa na Bodi. Hivyo bado tutaendelea na utaratibu wa Mhe. Rais kumtangaza au kumteuwa Mkurugenzi  Mkuu wa Mamlaka hiyo.

Kama Mamlaka imepewa nafasi ya kuruhusu utupaji taka baharini, kwa hivyo inaweza kutoa ruhusa ya kutupa taka za hatari kama za *nuclear*, ikatazwe kabisa kutupa taka baharini.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe napenda kueleza kwamba kuna Sheria ya *MARPOL* ya 73/78 ambayo Tanzania ni mwanachama imeelezea viwango vya taka vinavyoweza kutupwa baharini. Kwa hivyo kanuni zinazotungwa za udhibiti wa utupaji wa taka baharini kwa kufuata sheria za kimataifa, hivyo mamlaka haitaweza kuruhusu utupaji wa taka kinyume na sheria hizo.

Kifungu cha 27(2) Mhe. Said Ali Mbarouk alisema kwamba kinatoa uwezo wa kumkamata mtu, kirekebishwe kisije kikasababisha ugomvi

Mhe. Mwenyekiti, jibu ni kwamba utaratibu wa kukamata mtu anapofanya kosa ni jambo la kawaida, mfano kila siku raia wanakamata wezi na kuwakabidhisha kwa Polisi. Iwapo kutatokea kosa la jinai sheria hii haizuii mtu huyo kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria, kwa hivyo tunaona hakuna haja ya kukiondoa kifungu hicho.

Mhe. Said Ali Mbarouk pia alizungumzia kifungu cha 28 na 29 virekebishwa visije vikatoa adhabu kubwa kwa vyombo vidogo vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba vifungu hivyo havihusu vyombo vidogo vidogo bali vinahusu mtu anayeharibu kwa makusudi au kuhatarisha usalama wa vyombo.

Mhe. Said Ali Mbarouk pia alipendekeza kifungu cha 46 kibadilishwe ili watumishi wa Mamlaka watakaposababisha hasara wakati wakitekeleza majukumu yao mtumishi huyo alipe.

Mhe. Mwenyekiti, kikawaida vifungu kama hivi vinakuwemo kwenye sheria ili kutoa kinga kwa wafanyakazi wanapotekeleza majukumu yao kwa nia njema vyenginevyo wafanyakazi watakuwa wanaogopa kutekeleza majukumu yao. Pindipo mfanyakazi akibainika amefanya kosa kwa makusudi Mamlaka itamchukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Said pia aliendelea kwa kuelezea kwamba hakuna idadi ya wajumbe wa bodi katika jadweli, sifa na mwahala wanapotoka.

Mhe. Mwenyekiti, idadi ya wajumbe wa bodi ni 7, mwenyekiti, mkurugenzi Mkuu na wajumbe wengine watano, (imetajwa kwenye kifungu cha kwanza cha jadweli). Hata hivyo katika tafsiri ya Kiswahili ya mswada idadi hiyo

haikuandikwa kwa makosa jambo ambalo kamati imeshalirekebisha na sifa za wajumbe wote zimetajwa katika kifungu 1(3) ya jadweli. Ingawa sifa hizo sasa zitafanyiwa marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Ali Mbarouk pia alitaka ufafanuzi wa kifungu cha 4 cha Jadweli. Kifungu hicho kimejieleza vizuri hivyo namuomba Mhe. Mwakilishi akipitie tena atakielewa tu.

Pia alitaka kujua uanzishaji Mamlaka umezingatia nini?

Mhe. Mwenyekiti, tumeanzisha Mamlaka hii kwa kuzingatia mifumo ya wenzetu na kuona ni vyema mamlaka ikawa na usafiri wa baharini peke yake. Vile vile IMO inashauri kuanzisha Mamlaka ya usafiri wa baharini peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Ali Mbarouk pia alisisitiza kwamba maslahi ya wataalamu yazingatiwe vyenginevyo wataalamu watakimbia. Napenda nikiri kwamba tumepokea ushauri wake na tutaufanyia kazi.

Mhe. Abubakar Khamis alikuwa ni mchangiaji wa tatu.(Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni). Yeye mashaka yake au hofu yake ni kuhusu kufutwa kifungu 5 cha sheria *Maritime Transport Act* 2006 kinachoanzisha Mamlaka

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Umma inaweza kuanzishwa kupitia Sheria ya Baraza la Wawakilishi au kwa amri ya kuitawala *(Administrative Order)* ambayo chimbuko lake huwa ni katiba au sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Kupitia Sheria Nam 5/2006 kilichofanyika ni kuikasimu mamlaka ya Baraza kwa Mhe.Waziri. Lakini ilivyokuwa sasa Baraza la Wawakilishi limeamua kutumia uwezo wake wa kuanzisha taasisi, ipo haja ya kufanya marekebisho katika kifungu cha 5 cha Sheria Nam. 5/2006 ambacho kinampunguzia uwezo Waziri kuanzisha taasisi hiyo.

Hivyo, kupitia mswada huu wa sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini Zanzibar. Baraza sasa linaanzisha Mamlaka hii, hivyo inahitajika kufanya marekebisho katika kifungu cha 5 cha Sheria 5 ya 2006 na marekebisho hayo yasomeke kama ifuatavyo.

Kifungu cha 52(1) "kifungu cha 5 cha Sheria Nam. 5 ya mwaka 2006 kinafutwa na kifungu cha 52 (2) sasa kisomeke maneno "Mamlaka ya Usafiri Baharini yaliyopo katika Sheria ya Usafiri Baharini Nam. 5 ya mwaka 2006, yanafutwa na badala yake yaweko maneno ya Mamlaka ya Kusimamia Usafiri Baharini Zanzibar."

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na marekebisho hayo itabidi sasa kifungu cha 52 kiwe na vifungu vidogo 5 badala ya 4, Kifungu Nam. 52(3) sasa tunaomba kisomeke kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 6 cha Sheria ya Usafiri wa Baharini 2006 kinarekebishwa kwa kufutwa maneno iliyoanzishwa chini ya kifungu kilichopita na kifungu kilichokuwa 53(3) na (4) sasa kitakuwa ni kifungu kidogo 52(4) na (5).

Mhe. Mwenyekiti wa nne alikuwa ni Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini). Alitoa ushauri wa mambo yafuatayo:-

- Kuondolewa bandarini meli zilizokufa;
- *Speed boat* kufukuzana na kusababisha upotevu wa mizigo
- Upandaji wa nauli kiholela
- Taratibu za ukaguzi wa meli zifanyike kwa kipindi cha mwaka.
- Utaratibu wa mizigo katka *speed boat* zifuate utaratibu wa ndege.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa mambo hayo yatazingatiwa na yatashughulikiwa na Mamlaka.

Chombo cha bapa, vyombo vya kienyeji na vyombo vya kujifurahishia. Chombo cha bapa ni chombo kilichokuwa hakina mkuku kama tishali. Vyombo vya kienyeji ni "*native vessels*" ambayo ni majahazi na vyombo vya kujifurahishia ni vyombo vya starehe "*Pleasure crafts"*

Alitaka kujua kusajili rehani na kinga ya uchafuzi ya bahari inafanywa vipi na Mamlaka.

Usajili wa rehani "*mortgage*" unasajiliwa kwa taratibu zilizoelezwa katika sheria Nam. 5 ya 2006 na Kinga ya Mazingira itatekelezwa na Mamlaka kwa kufuata kanuni za sheria ya kimataifa ya *MARPOL* 73/78 chini ya sheria Nam .5 ya mwaka 2006

Pia alishauri adhabu ziwekwe kwa fedha ya Tanzania badala ya fedha za kigeni. Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba adhabu zimewekwa kwa kulipa kwa shilingi kwa thamani ya dola. Dola hapa imewekwa tu lakini wote watalipa kwa shilingi lakini watakaotaka kulipa kwa dola ataruhusiwa lakini thamani ya dola itakuja kwenye shilingi.

Mhe. Abass Juma Muhunzi (Mwakilishi wa Jimbo la Chambani) anauliza kwa nini imeelezwa meli za serikali maana yake ni meli ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tafsiri hiyo ya "Meli za Serikali" ambayo imeelezwa vizuri katika kifungu cha Tafsiri na sio tafsiri ya

Serikali. Lengo hasa la kuweka tafsiri hii kutoa msamaha kwa meli za SMZ, SMT na meli za Serikali za kigeni zinazokaribishwa nchini na SMZ kwa ajili ya kufanya shughuli ambazo zinatambuliwa na kuruhusiwa na SMZ.

Pia alitaka kuelewa eneo la bahari ya Zanzibar yamefutwa kivipi? Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hili nimeshalijibu wakati nikimjibu Mhe. Saidi Ali Mbarouk kwamba hatukufuta kwa sababu sheria ya 2006 inaelezea na Katiba ya Zanzibar inaelezea mipaka ya Zanzibar kwenye maji.

Lakini pia alitaka kujua vipi tutaweza kujiendesha Kimataifa kwenye shughuli za meli na kesi zake?

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kwa sasa ina uwezo mkubwa wa kusimamia mambo ya kimataifa yanayohusiana na meli. Hatua hii imefikiwa baada ya kuwasilishwa IMO kazi zitakazofanywa na Zanzibar katika mikataba mbali mbali ya kimataifa.

Mara nyingi kesi za meli katika masuala ya baishara ni “civil case” hivyo mtu yeyote aliyeonewa anaweza kushitaki. Mwaka 1997 meli ya *Global* iligonga gati ya Zanzibar, serikali ilifungua kesi dhidi ya meli hiyo ambayo ilikamatwa Panama ambapo Serikali ilishinda kesi hiyo kwa kupitia wataalamu wake.

Hivyo SMZ ina uwezo wa kujisimamia katika kesi zake na kushinda. Kama ulivyosema mwenyewe jana Mhe. Mwenyekiti, wewe ulikuwa mjumbe wa Bodi na nyiye Bodi Shirika la Bandari ndiyo mlioishauri serikali na tukaweza kushinda kesi hiyo. Kwa hivyo tunao uwezo wa kusimamia kesi bila ya matatizo yoyote.

Pia alitaka kujua jee  upo uhusiano wakati wa kukabiliana na majanga?

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba shughuli za uokozi zinafanywa kwa mashirikiano na taasisi nyengine kuanzia vikosi vya ulinzi, makampuni ya meli na ndege, watu binafsi na taasisi yeyote ambayo itaonekana inaweza kutoa msaada. Kifungu cha 18 kinaelezea mtu au taasisi yoyote inaweza kushirikishwa pale inapotokea ajali na katika kutekelezwa kifungu hicho kutakuwa hakuna maingiliano ya majukumu. Mamlaka itaratibu shughuli zote za uokozi baharini.

Pia alitaka kujua iwapo kuna wataalamu wa kutosha wenye sheria za baharini.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tuna wataalamu wa kutosha wenye fani ya *Maritime*:-

| | |
|---|---|
| *Maritime administration* | *7* |
| *Maritime law* | *2* |
| *Shipping management* | *2* |
| *Port management* | *2* |

Bado tunaweza kuwaajiri wataalamu wengine itakapoonekana kuna haja ya kuanya hivyo. Lakini ili kuwaajiri zaidi basi ni lazima tuanzishe chombo kama hichi kwa sababu hatuwezi kuwaajiri watu ambao tunatakuwa hatuutumii utaalamu wao, lakini tukianzisha Mamlaka mahitaji yetu yatakuwa makubwa zaidi na sisi kama Mamlaka na Wizara tutaendelea kutafuta wataalamu zaidi ili kuimarisha Mamlaka yetu kwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji wa sita alikuwa ni Mhe. Salmin Awadh (Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni). Yeye alizungumzia kuhusu kifungu Nam 5 cha sheria namba 5 ya 2006 alisema kwamba kisifutwe kwa kuwa kinampa uwezo Mhe. Waziri kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa usalama baharini. Mamlaka hiyo kupitia mswada huu inachukuliwa na Baraza la Wawakilishi na ndio maana tukakifuta kifungu hicho.

Pia alitaka kuwe na bima kwa vyombo vya baharini na kupanda na kushuka kwa nauli za abiria kudhibitiwe. Tumepokea ushauri wake wa mambo ya Bima na nauli za abiria tutashughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mheshimiwa alitaka kuelewa Mkurugenzi Mkuu hakupewa kazi katika Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu imeelezwa kuwa ndie mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Mamlaka kifungu 8(3) na kwa kuwa kazi za Mamlaka zimetajwa katika kifungu 5 yeye ndie msimamizi mkuu wa majukumu ya Mamlaka. Kwa hivyo utakaposoma majukumu ya Mamlaka utaona wajibu wa Mkurugenzi Mkuu katika majukumu hayo.

Lakini pia Mhe. Salmin amesema waziri amepewa madaraka makubwa kubadili jadweli.

Ufafanuzi ni kuwa waziri ataweza kubadili jadweli baada ya kushauriana na Bodi. Sio waziri peke yake akurupuke na aseme kama hili nalibadilisha au hili. Waziri atashauriana na bodi ndio yatafanyika marekebisho yale yaliyosemwa kwenye jaduweli.

Kuhusu sifa za wajumbe. Nakubaliana na Waheshimiwa wengi ambao wamechangia kwamba tusiwe na sifa maalum kwa wajumbe wa bodi na sasa kifungu hichi kinafanyiwa marekebisho na kwamba waziri atateuwa wajumbe watano kama atakavyoona yeye inafaa.

Mhe. Ame Ussi Juma (Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi), kuhusu elimu ya watendaji, udhibiti wa meli za kigenim mapato, doria kwenye eneo la Zanzibar. Ushauri wa Mheshimiwa tumeupokea na tunamshukuru sana na tutaufanyia kazi.

Mhe. Ame Mati Wadi (Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe) alikuwa ni mwakilishi wa nane katika kuchangia. Yeye zaidi alichangia kuhusu minara kuwa na utaratibu mwengine na aliuliza je, minara inalipiwa na nani? Minara na maboya yako chini ya Shirika la Bandari na matengenezo yake yote yanafanywa na Shirika la Bandari. Kuhusu vyombo vidogo vidogo kukaguliwa katika bandari ndogo. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi Ame Mati Wadi kwamba wizara yangu inakubali wazo lake.

Kitengo cha Mrajis wa Meli kimeanza kazi ya kuvikagua vyombo vidogo katika bandari ndogo ndogo na Mamlaka itafanya hivyo kwa kuvifata vyombo hivyo huko viliko.

Mhe. Makame Mshimba (Mwakilishi wa Jimbo la Kitope) alikuwa ni mchangiaji wa tisa. Alizungumzia kuhusu masharti ya wajumbe wa bodi, nimeshasema kwamba masharti hayo yameshaondolewa. Kwa hivyo asiwe na wasiwasi.

Kuhusu kampuni ya *Danaos* kwamba kuna mabaharia wanachukuliwa na wanapelekwa nje. Ni kweli kuna Kampuni hiyo inafanyakazi kihalali ambapo huajiri vijana wetu kwa lengo la kuwapatia ajira katika meli za kigeni kwa kupitia afisi ya Mrajis wa Meli na *Seaman Union.* Yaani wale *Danaos* wakisha kutafuta vijana kabla ya kuwapeleka nje ni lazima waonane na Mrajisi wa meli ili wapate urajisi wao. Lakini pia na *Seaman Union* ishirikishwe katika kuwatambua hao mabaharia watakaokwenda nje ya nchi. Wakishakuwapeleka wakipotea au wakitoroka nafikiri huwa wanaripoti katika Balozi zetu. Kama ilivyo kawaida mtu yeyote ambaye anazamia nje Ubalozi na Nchi husika huwa zinashughulikia katika kuwarejesha na kuwachukulia hatua za kisheria.

Kuhusu mfanyakazi aliepata kifafa akaangukia baharini. Mhe. Mwenyekiti, napenda nikiri kwamba ripoti kama hizi hufanyiwa uchunguzi na kulipwa fidia, ambapo Mamlaka hii itakuwa ni jukumu lake kufuatilia kesi kama hizi. Hivi sasa bado hatujapata kesi kama hii lakini ikitokezea tutaifanyia kazi na atalipwa fidia kama anastahiki kufanyiwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia alizungumzia kwamba vyombo vidogo vidogo vinagongwa sana baharini. Ni kweli lakini kuna sehemu mbili. Kuna sehemu moja wakati mwengine makosa yanakuwa kwa vyombo vyenyewe vidogo vinatembea bila ya taa. Lakini upande mwengine makosa huwa kwa hizi meli kubwa. Linapotokea tatizo kama hili uchunguzi hufanywa na ikithitibika waliogonga ndio wenye makosa basi waliogongwa wanalipwa fidia ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa wa kumi katika kuchangia ni  Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani). Tunamshukuru sana kwa mchango wake wa busara, alisisitiza kwamba Mamlaka ipatiwe vitendea kazi, maslahi ya wafanyakazi yawe bora na bodi kufanyakazi kwa uadilifu. Tunamuahidi kwamba mambo hayo tutayafanyia kazi, tutalinda sana maslahi wa wafanyakazi wetu, tutatafuta vitendea kazi lakini tutachagua bodi ambayo itafanya kazi kwa uwadilifu.

Mhe. Ali Denge Makame (Mwakilishi wa Jimbo la Amani) alizungumzia udhibiti wa mabaharia na mafao yao. Neno “Udhibiti” maana yake sio kwamba tusiajiri mabaharia maana yake ni kwamba ikiwa tutaajiri mabaharia ambao watafanyiwa usaili, watapewa kazi, watashughulikiwa vizuri ili na maslahi yao yawe mazuri. Uwajiri wa utaendelea kila tutakapopata nafasi kwa meli zetu za ndani. Lakini pia Malaka kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali za kibinafsi zitakuwa chachu ya kutafuta nafasi za mabaharia ili wananchi wetu waendelee kupata ajira za ziada.

Pia alitaka kujua uwezo wa Shirika, Mamlaka na Bodi. Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada huu hakuna neno Shirika ila kuna Mamlaka inayoongozwa na bodi. Kwa hivyo Mamlaka ipo itaongozwa na bodi ya Wakurugenzi ndiyo itakayokuwa ina kauli ya mwisho.

Mhe. Ali Mzee Ali (Mwakilishi wa kuteuliwa Jimbo la Ikulu) alikuwa ni mchangiaji a kumi na mbili. Napenda nikiri kwamba alitoa mchango mzuri sana na umetusaidia sana, mchango wake tunauheshimu sana kwa sababu pia na yeye ni mtaalamu kidogo wa mambo haya ya baharini, japo hakutaka kusema wazi wazi.

Alitaka kujua sheria ya Nam. 5 ya 2006 na Mswada huu wa Sheria hii.  Mhe. Mwenyekiti, Sheria Nam 5 ya 2006 ni matakwa ya Waheshimiwa Wawakilishi baada ya kukataa kuanzishwa kwa sheria ile ya Bara. Na Waheshimiwa Wawakilishi kwa pamoja waliomba kwamba Zanzibar iwe na sheria yake ya kusimamia usafiri wa baharini ambayo tulianzisha sheria ile Nam. 5 2006 na baadaye sheria ile ikatutaka tuanzisshe chombo cha kusimamia sheria ile ndiyo huu Mswada tuliouleta leo ambao tunatarajia kwamba utapitishwa ili tuwe na kitu cha uhakika.

Pia Mhe. Ali Mzee Ali alisema kuwa Zanzibar hakuna wataalamu wa *first class Marine Engineer na First Class Master Mariner*. Ukweli ni kwamba wataalamu hao wapo ingawa ni wachache na mmoja wapo amepewa jukumu na Serikali ya kukagua meli zinazosajiliwa Zanzibar, wapo wataalamu wawili tunaowatambua.

Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban (Waziri wa Utawala Bora) na yeye tunamshukuru kwa ushauri na busara na kutuongoza katika mambo ya sheria na tumeupokea sana ushauri wake zaidi katika kufuta kifungu cha sheria Nam. 5 na Kifungu cha 52(2).

Mheshimiwa wa mwisho aliyechangia Mswada ule alikuwa ni Mhe. Mzee Ali Ussi (Mwakilishi wa Jimbo la Chaani na ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi) na yeye namshukuru sana, kwa sababu jana alipopata nafasi alijibu baadhi ya hoja za Mhe. Ame Mati na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima ili kupitia Mswada kifungu baada ya kifungu.

**KAMATI YA BARAZA ZIMA**

| | |
|---|---|
| Kifungu cha 1 | Jina Fupi na Tarehe ya Kuanza Kutumika |
| Kifungu cha 2 | Ufafanuzi Pamoja na Marekebisho Yake |
| Kifungu cha 3 | Kuanzisha kwa Mamlaka Pamoja na Marekebisho yake |
| Kifungu cha 4 | Eneo la Udhibiti na Mamlaka Pamoja na Marekebisho Yake |
| Kifungu cha 5 | Majukumu ya Mamlaka Pamoja na Marekebisho yake |
| Kifungu cha 6 | Uwezo wa Mamlaka. |
| Kifungu cha 7 | Bodi ya Wakurugenzi. |
| Kifungu cha 8 | Mkurugenzi Mkuu Pamoja na Marekebisho Yake |
| Kifungu cha 9 | Uwezo wa Waziri. |
| Kifungu cha 10 | Uwezo wa Bodi. |
| Kifungu cha 11 | Uwezo wa Mkurugenzi Mkuu. |
| Kifungu cha 12 | Uchunguzi wa Ajali Baharini |
| Kifungu cha 13 | Mabaki ya Meli. |
| Kifungu cha 14 | Uchafuzi wa Mazingira Baharini. |

| | |
|---|---|
| Kifungu cha 15 | Usalama wa Baharini. |
| Kifungu cha 16 | Ulinzi wa Nchi. |
| Kifungu cha 17 | Taratibu za Uendeshaji wa Shughuli za Usalama |
| Kifungu cha 18 | Utafutaji na Uokoaji Baharini Pamoja na Marekebisho yake |
| Kifungu cha 19 | Fedha za Mamlaka Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 20 | Haki Kutokana na Huduma na Vifaa Vilivyotolewa Kabla ya Wizara na Usafiri na Taasisi Nyengine Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 21 | Utoaji wa Baadhi ya Mali Kwenda kwa Mamlaka Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 22 | Uwezo wa Kukopa Fedha Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 23 | Mwaka wa Fedha Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 24 | Bajeti ya Mwaka na ya Ziada. |
| Kifungu cha 25 | Hesabu na Ukaguzi. |
| Kifungu cha 26 | Taarifa ya Mwaka |
| Kifungu cha 27 | Uharibifu wa Mali ya Mamlaka Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 28 | Kutoa huduma au Vifaa Bila ya Kibali Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 29 | Kuhatarisha Usalama wa Chombo Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 30 | Uzembe, Kushindwa Kutoa Maelezo au Kutoa Maelezo ya Uongo Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 31 | Makosa Yanayohusiana na Usalama wa Vyombo Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 32 | Usumbufu au Kupinga Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 33 | Kutokufuata Maagizo Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 34 | Kumwaga Taka Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 35 | Adhabu ya Jumla Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 36 | Makosa kwa Taasisi . |
| Kifungu cha 37 | Makosa Yanayoweza Kudanganywa Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 38 | Dhana ya Mamlaka Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 39 | Shitaka kwa Sheria Nyengine Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 40 | Uwezo kwa Makosa Yanayofanana. |
| Kifungu cha 41 | Faini Kulipwa kwa Mamlaka. |
| Kifungu cha 42 | Uwezo wa Kuweka Kizuizini Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 43 | Wajibu wa Fidia kwa Mamlaka Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 44 | Utoaji wa Huduma na Vifaa au Mtu Mwengine Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 45 | Msamaha wa Kutokichukua na Kukamatwa Mali Pamoja na Marekebisho Yake. |

| | |
|---|---|
| Kifungu cha 46 | Ushauri, Maelekezo au Msaada wa Chombo. |
| Kifungu cha 47 | Uwezo wa Kuingia Katika Ardhi na Jengo |
| Kifungu cha 48 | Ushahidi wa Kitambulisho Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 49 | Malipo, Hasara na Faida. |
| Kifungu cha 50 | Kanuni Pamoja na Marekebisho Yake. |
| Kifungu cha 51 | Uwezo wa Waziri Kutoa Maelekezo. |
| Kifungu cha 52 | Marekebisho ya Sheria Nam. 5 ya Mwaka 2006 Pamoja na Marekebisho Yake. |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima umeupitia Mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**Mswada wa Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri Baharini ya Mwaka 2009**

*(Kusomwa kwa mara ya Pili)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kw
amba Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2009, usomwe kwa mara ya pili.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**TAARIFA MAALUM**

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kipindi chote hichi. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza wote ambao walishiriki katika maandalizi, katika mazishi ya mwenzetu Mhe. Daud Hassan Daud.

Vile vile ile Kamati ambayo niliiunda mimi ya Mhe. Soud Yussuf Mgeni, Mhe. Said Ali Mbarouk, Najma Khalfan, Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) walifanya kazi nzuri sana kwa niaba yetu. Kwa hivyo, kwa niaba yenu na Baraza tunawashukuru sana na kamati ile imeshavunjwa na Ishalla haitoundwa tena mpaka Baraza limalizike.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, kwa kuwa shughuli hizi zimemalizika kwa salama na amani toa hoja jioni leo tusije na Baraza tuliahirishe mpaka siku ya Ijumaa tarehe 30 asubuhi.

## KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa busara na hekma zako baada ya kuwaona Waheshimiwa wamefanya kazi nzito ya kuweza kupitisha Miswada mbali mbali na kwa kuwa leo shughuli zetu zimemalizika mapema umeona utumie busara kwamba tuliahirishe Baraza lako mpaka siku ya Ijumaa.

Kwa hivyo kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza lako tukufu hadi siku ya Ijumaa terehe 30, saa tatu asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 6:45 mchana Baraza liliakhirishwa hadi*
*tarehe 30/1/2009 Saa 3:00 za asubuhi)*